**MWANGWI** kila kona uwekezaji wa bandarini

UKURASA 2



**BASHE** na CCM washtuka malipo wakulima tumbaku kucheleweshwa

UKURASA 3




UKURASA 11


# Nipashe

Jumatatu Julai 3, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581360

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


RIPOTI YA UCHUNGUZI

# Mjamzito abakwa, afungwa katika kiroba

**APEWA** dawa za kuzuia VVU bila maelekezo, azi-tupa; maswali yatawala PF3 ilivyojazwa... *Endelea ukurasa wa 4 & 19*



UKURASA WA 17

## DK. MWINYI AONYESHA MWANGA WAWEKEZAJI ZANZIBAR



RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema atawasaidia wawekezaji wanaokumbana na vikwazo na changamoto mbalimbali ili kufanya biashara zao nchini.

UKURASA WA 19

## PSSSF YAHADHARISHA WASTAAFU DHIDI UTAPELI

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), umewatahadharisha wanachama wao wastaafu kuwa makini na utapeli mpya uliojitokeza na kusababisha baadhi yao kuibiwa fedha zao kwenye akaunti bila wao kujijua...

UKURASA WA 19

## LATRA KUZUNGUMZA NA TIRA WANAOPATA AJALI SAFIRINI WALIPWE FIDIA

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), imesema inafanya mazungumzo na TIRA ili abiria wanaopata ajali kwenye mabasi safarini wawe wanalipwa...

KESI MAGUNIA YA MKAA

## 'Nilitumia saa tano kuuchoma mwili wa mke wangu, kichwa kiliungua kirahisi'

UKURASA 3

# Kicheko kampuni za simu zikifuta tozo kutuma fedha

UKURASA 2



MICHEZO YANGA SC KUIBOMOA TENA ASEC MIMOSAS UK. 24

KATUNI UK. 6

# Mwangwi kila kona uwekezaji bandarini

**Na Mwandishi Wetu**

MJADALA kuhusu uendeshaji wa Bandari baina ya serikali za Tanzania na Dubai, umeanza kutoa picha ya hatua za kuchukuliwa ili nchi ifaidike na uwekezaji huo.

Baada ya suala hilo kuanza kusambaa kwenye mitandao ya kijamii, Juni 10, mwaka huu, Bunge liliridhia Azimio la Mkataba wa Ushirikiano baina ya nchi hizo mbili (IGA).

Mjadala ulijielekeza kwenye vifungu vya kisheria vinavyoonyesha huenda Tanzania isifaidike; na wakati mwingine kukiwapo pia na tuhuma za ubaguzi na masuala ya Muungano miongoni mwa waliojadili. Kauli za karibuni za viongozi wa dini, wasomi, viongozi wengine wa serikali, chama, mashirika yasiyo ya kiserikali na wadau wa bandari na wanasiasa mashuhuri zimeanza kuondoa ukungu.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, wakati akihitimisha kikao cha Bunge wiki iliyopita jijini Dodoma, aliirudia pia kwenye tukio la Baraza la Iddi jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki iliyopita kuwa serikali itachukua maoni na ushauri uliotolewa na wananchi mbalimbali kuhusu suala hilo, lengo ni kuhakikisha hakuna anayeachwa nyuma.

Wasomi nguli wa sheria nchini, Profesa Issa Shivji, alizungumza kuhusu suala hilo na kusema kinachotakiwa kufanyika sasa ni marekebisho yatakayofuta azimio hilo la awali la Bunge na kutengeneza lingine litakalojumuisha maoni ya wananchi kwa kadri mijadala inavyoendelea.

Kabla ya hoja hiyo ya Shivji, Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo na Mbunge wa zamani wa Kigoma, Zitto Kabwe, alisema serikali inaweza kufanya nyongeza ya azimio hilo na kuiwasilisha kwa wenzao wa Dubai. "Pamoja na kwamba IGA imesainiwa, serikali yetu inaweza kuwasilisha kwa serikali ya Dubai mapendekezo ya maboresho ya maeneo ya mkataba kutokana na maoni ya wananchi. Wabunge walipaswa kutaka maboresho ya IGA na kuridhia baada ya hapo. Sasa, ni wajibu wa Serikali kuandaa jedwali la maboresho ya IGA na kupata 'addendum'," aliandika Zitto katika mojawapo ya magazeti ya mitandaoni nchini.

Mkurugenzi wa Huduma za Sheria wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mohamed Salum, alisema azimio lililopitishwa na Bunge halina tofauti kubwa na lililopitishwa kuhusu bomba la mafuta baina ya Tanzania na Uganda na masuala mengi yanayohojiwa yakiwamo ya ukomo wa mkataba na mgawanyo wa faida yatakuwa ndani ya mkataba wa uwekezaji na maoni na ushauri unaotolewa yatazingatiwa na serikali.

Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS), kilichounda timu ya wataalamu kuchambua na kubainisha maeneo yanayohitaji kutazamwa kwa kina na serikali endapo itaingia mikataba ya uwekezaji na kampuni ya DP World.

Uchambuzi wa TLS ulijibu hoja mbili kubwa; mosi kuhusu mkataba huo haujaipa Dubai haki za kipekee kuhusu bandari zote za nchini na kwamba Tanzania bado itaruhusiwa kufanya kazi na wabia wengine na pili kuhusu sababu za kuwepo kwa vipengele vya kulinda haki za mwekezaji pale serikali itakapoamua kutaifisha bandari au uwekezaji mwingine ulio kwenye makubaliano.

TLS pia ilitoa ushauri katika maeneo makubwa mawili; kwenye vifungu vya 23 (3) na 23 (4) ilipendekeza kuwapo kwa mazingira ambayo mkataba huo unaweza kuvunjwa na upande utakaoona inafaa. Hii ni kuondoa dhana kwamba mkataba hautavunjika. La pili lilihusu kutumika kwa sheria za Tanzania katika utekelezaji wa mkataba huu.

Katibu wa Baraza la Maaskofu wa Tanzania (TEC), Dk. Charles Kitima, mmoja wa wachangiaji waliokuwa na hofu ya namna gani taifa litafaidika na uwekezaji wa kigeni zaidi ya nusu karne baada ya kuwa tumejitawala na kwamba dhana kuwa Watanzania hawawezi na wageni tu ndiyo wanaweza ni mojawapo ya changamoto kubwa.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dk. Eliezer Feleshi, akifafanua masuala mbalimbali ya IGA aliwatoa hofu Watanzania kuhusu mkataba huo huku akieleza kuwa wamejiridhisha vya kutosha na kwamba hakuna kipengele cha miaka 100 na kwamba utaratibu mzuri umewekwa ikiwamo pande hazitaelewana.

Feleshi alikanusha madai kuwa Tanzania haitaweza kujitoa katika makubaliano hayo na kwamba bandari yote ya Dar es Salaam imeuzwa kwa kufafanua kuwa mpaka sasa Mamlaka ya Bandari za Tanzania (TPA) haijaingia makubaliano au mkataba wowote na DP World.

Mwanasheria wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Kulwa Mumbili, alisema mchakato wa IGA ni mrefu na unahusisha wataalamu wengi wenye weledi kwa nia ya kuhakikisha maslahi ya nchi yanazingatiwa kikamilifu.

Katika mapendekezo yake, Zitto alishauri kuundwa kwa kampuni ya Kitanzania itakayochangiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA), Mifuko ya Hifadhi za Jamii na kupitia Watanzania kwenye hisa zitakazouzwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE).

Kampuni hiyo, kwa mujibu wa Zitto, ndiyo itatakiwa kuingia makubaliano ya uendeshaji wa bandari za Tanzania kwa ushirikiano wa asilimia 50 -50 na kampuni ya DP World – jambo litakalosababisha mgawanyo unaofanana wa faida, kuongeza uwezo wa Watanzania kuendesha shughuli za bandari kisasa na faida nyingine.



Meneja Uhusiano na Elimu kwa Wanachama PSSSF, James Mlowe (kulia), akimhudumia mwanachama wa mfuko huo, Osmud Xavery kwenye banda la PSSSF viwanja vya maonesho Sabasaba jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kicheko kampuni za simu zikifuta tozo kutuma fedha

**Na Halfani Chusi**

MAUMIVU yaliyokuwa yanalalamikiwa na wananchi kuhusu tozo kwenye miamala ya kielektroniki yameondoka, baada ya kampuni za simu za mkononi nchini kuanza utekelezaji wa kupunguza gharama hizo kuanzia Julai Mosi, mwaka huu.

Hatua hiyo imekuja ikiwa ni siku chake tangu serikali kupitia Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, kutangaza bungeni kufuta tozo kwenye kila laini ya simu ifikapo Julai Mosi.

Waziri Mwigulu alisema lengo kuu la utekelezaji huo ni kuchochea matumizi ya kielektroniki katika miamala mbalimbali.

Hatua hiyo ililazimu Nipashe kupiga hodi katika kampuni za simu za mkononi ili kuona utekelezaji wa agizo hilo, sambamba na kuzungumza na baadhi ya Watanzania kupata maoni yao.

Mkurugenzi wa Uhusiano na Mawasiliano, Vodacom Tanzania, Zuweina Farah, alisema kampuni hiyo tayari imeshaondoa huduma hiyo na tayari wateja wake wanaendelea kufurahia huduma bila tozo.

Alisema kuondolewa kwa tozo kutaleta athari chanya kwenye upokeaji wa huduma za fedha kupitia simu za mkononi na hivyo kuchochea ujumuishwaji wa kifedha.

"Kwa kuondoa tozo, gharama zinazohusisha kutuma na kupokea pesa kupitia majukwaa ya pesa za simu zinapunguzwa, hii itachochea wananchi kutumia huduma za pesa katika shughuli zao za kifedha za kila siku.

"Kama vile kutuma pesa kwa familia, kulipa bili au kufanya manunuzi na hivyo kuendeleza zaidi ajenda ya serikali ya kuhakikisha wananchi wanatumia pesa mtandao," alisema Zuweina.

Vile vile, alisema kuwa huduma ya kifedha kwa kutumia simu ina uwezo wa kutoa huduma mbalimbali, ikiwa ni pamoja na akiba, mikopo na bima akisisitiza kuwa kupokelewa kwa huduma hizo kunaweza kusaidia watu waliokuwa wameachwa nje ya mfumo rasmi wa kifedha ili kushiriki katika kujenga uchumi, kuwekeza na kujiwekea bima ili kupambana na hatari kwa ufanisi zaidi.

Ofisa Mkuu wa Tigo, Angelica Tesha, amesema uamuzi wa serikali kuondoa tozo umepokelea vizuri ni hatua nzuri ya kwenda na ulimwengu wa kidigitali, amesema kampuni hiyo itaendelea kufanya kazi na serikali kuhakikisha huduma za kifedha zinakuwa nafuu kwa Watanzania.

Akizungumza kwa njia ya simu, Meneja Uhusiano wa Airtel, Jackson Mmbando, alisema walilipokea agizo hilo na wanalifanyia kazi kuanzia kesho (leo) watakuwa na majibu kamili.

"Agizo limetoka jana (juzi) kwa hiyo tunaangalia namna ya kuondoa huduma hiyo na mchakato utakapo kamilika tutawataarifu wateja wetu, kwa sasa siwezi kulizungumzia sana suala hilo, kwa sababu linafanyiwa kazi.

"Kuanzia kesho (leo), nitakuwa nina majibu sahihi na kuweza kulizungumzia hilo, agizo halijatolewa muda mrefu kwa hiyo lazima kuna mchakato ufanyike ili kuiondoa huduma hiyo lakini tunalishughulikia," alisema.

Naye Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alisema serikali ilikubali kuondoa tozo kwenye miamala ili kuwapa wananchi unafuu kwenye miamala ya kifedha.

"Kama mnakumbuka suala la tozo lilikuwa na kelele kidogo, wakati ninaingia ilikuwa asilimia 100, tukapambana huku na kule serikali ikatuelewa tukaenda hadi asilimia 50, juzi Rais Samia Suluhu Hassan ametuelewa ameondoa imekuwa sifuri kabisa," alisema.

**WATUMIAJI WANENA**

Zuhura Ramadhani, anayetumia Mtandao wa Vodacom, alisema alipokea ujumbe kwenye simu yake unaothibitisha kuondolewa kwa tozo, kwamba hata alipofanya miamala yake ya kutuma hakukatwa.

Mtumiaji mwingine Jakobo Saidi, alisema ameona mabadiliko kwenye miamala aliyoifanya ya kutuma na kupokea fedha yake ikiwamo makato kidogo kutokana na kuondolewa kwa huduma hiyo.

# HABARI KITAIFA



Mkufunzi kutoka Chuo Kikuu Dodoma (UDOM), Idara ya Uhandisi, Dk. Ombeni Mdee, akieleza pampu ya maji inayotumia umeme mdogo, iliyobuniwa na chuo hicho ili kupunguza matumizi ya nishati hiyo, katika Banda la UDOM, kwenye Maonesho ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (DITF) jana. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

KESI MAGUNIA YA MKAA

## 'Kichwa cha mke wangu kiliungua kirahisi'

**Na Grace Gurisha**

MFANYABIASHARA Khamis Luwonga (38), anayetuhumiwa kumuua mkewe Naomi Marijani na kumchoma moto kwa kutumia magunia mawili ya mkaa, amedai katika maelezo yake ya onyo kuwa kichwa cha mkewe kiliungua kirahisi sana kwa sababu alipokuwa anamchoma alikuwa anakigeuza.

Amedai kuwa alianza kuuchoma mwili wa mke wake kuanzia saa tano asubuhi hadi saa 10 jioni, kwa sababu anakumbuka siku hiyo mtoto wake alirudi toka shuleni wakati yeye anamalizia kuuchoma mwili huo.

Pia alidai kuwa nyama za sehemu za siri, maziwa na makalio zilichelewa kuungua na kuisha haraka kwa sababu zilikuwa na mafuta mengi, lakini mafuta hayo yalisaidia moto kuwaka.

Maelezo hayo ya onyo na ya mlinzi wa amani yalisomwa mwishoni mwa wiki na Wakili wa Serikali, Mosie Kaima, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Ramadhani Rugemalila wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam.

Luwonga katika maelezo yake hayo, anadai kuwa watu wasingeweza kusikia chochote kwa sababu karibu na nyumbani kwake kuna Kanisa la Efatha na watu walikuwa wamejaa kanisani wanaendelea na ibada.

Anadai kuwa kutokana na mgogoro wao wa ndoa, yeye na mkewe walikaa miaka miwili kila mtu analala chumbani kwake na pia hakukuwa na tendo la ndoa kati yao.

Walikuwa wanaishi nyumba ya ghorofa moja, mmoja anakaa chini mwingine juu.

"Siku ya tukio Mei 15, 2019 nilirudi nyumbani asubuhi, nilala nje ya nyumba yangu kwa siku tano (kwa Magreth), nilimkuta mke wangu akimwandaa mtoto ili aende shuleni.

"Hii ilikuwa ni kawaida kurudi nyumbani asubuhi, kwa sababu hata yeye huwa anafanya hivyo, ilifikia wakati kila mtu anatoka analala nje bila kutoa taarifa kwa mwenzake na siku hiyo nilimwuliza mke wangu anataka nini ili nimwache," alidai Luwonga.

Anadai kuwa aliacha simu yake, ghafla iliita ambapo jina lililotokea lilikuwa la mwanamke, mke wake alichukua simu hiyo na kuanza kumgombeza kuwa wanawake zake wanapiga simu, ugomvi ukaanza.

Anadai kuwa wakati wanaendelea kugombana, alimshika mke wake na kumweka kitandani ili aache ukorofi.

"Naomi alinivuta sehemu zangu za siri kwa nguvu, nilipata maumivu makali ndipo nilipompiga na kumsukuma kwa bahati mbaya ukutani akajigonga karibu na mlango wa chooni," anadai.

Anadai kuwa mkewe alivuja damu nyingi kichwani na kufariki dunia papohapo na kwamba maneno yake ya mwisho yalimchanganya sana, akaanza kufikiria ataufanyaje mwili huo.

Anadai jambo la kwanza alifikiria kwamba auzike mwili nyumbani, lakini alifikiria ndugu wakija wanaweza kujua. Akafikiria tena, nyumbani kwake kuna magari manne, achukue gari moja aubebe mwili akautupe, lakini aliwaza njiani huenda akakutana na trafiki.

"Nikapata wazo la kumchoma moto kwa kutumia kuni, lakini nikasema kuni zitatumika nyingi sana, kwa hiyo nitumie mkaa, lakini nikasema majivu yakibaki hapa itakuwaje? Kwa sababu Naomi atakuwa anaendelea kutafutwa wakija kupima majivu wakajua ni ya mke wangu nitafanya je?

"Kwa hiyo, nilipata wazo kwamba nitamchoma moto na majivu nitakwenda kuyafukia shambani kwangu Mkuranga," alidai mshtakiwa katika maelezo yake ya onyo.

Alipoulizwa na askari aliyekuwa akimchukua maelezo hayo kuwa kwa nini hakwenda kutoa taarifa Kituo cha Polisi, alidai alishawahi kwenda kushtaki mara kadhaa, lakini walimwambia "huyo ni mke wako".

"Kuna siku mke wangu alinichoma na kisu mkononi nikaenda kituo cha polisi, nikaambiwa niondoke, huyo ni mke wangu, pia alishawahi kunivuta sehemu zangu za siri mbele ya mama yangu, hakuishia hapo tu alishawahi kunipiga na ndoo ya chooni mbele ya wapangaji wangu.

"Yaani ugomvi huu ulikuwa mkubwa sana hadi nikaingia uoga wa kula chakula nyumbani wala kulala nyumbani kwa sababu nilikuwa ninaogopa kuwekewa sumu, tulifikia kwenye hatua mbaya sana," anadai.

Anaendelea kudai ni hali iliyomfanya awe na uoga hata kutoa taarifa kwa ndugu kwa sababu wangejua kuwa amelipiza kisasi kutokana na mambo aliyokuwa akifanyiwa na Naomi.

"Mke wangu alikuwa na mwanaume mmoja hivi ndiye aliyesababisha sisi kugombana, kwa sababu ilifikia hatua Naomi ananiambia kuwa huyo mtu wake ndiyo ana fedha kushinda yeye.

"Ugomvi wetu huu familia zetu zilikuwa zinaujua, walijitahidi sana kutusuruhisha, lakini ilishindikana," anadai.

Katika maelezo hayo, inadaiwa kuwa wakati mwili ukiendelea kuungua, mshtakiwa alichukua simu ya mke wake na kuanza kujitumia ujumbe.

"Kwa sasa nimeamua kuokoka na kumrudia Mungu ndiyo maana nimezungumza ukweli bila kupindisha mambo," anadai.

Katika kesi hiyo ya mauaji Na. 4 ya mwaka 2019, mshtakiwa Luwonga ambaye ni Mkazi wa Kigamboni, Dar es Salaam, anadaiwa Mei 15, 2019, akiwa Gezaulole, Kigamboni, alimuua Naomi Marijani.

KUCHELEWA MALIPO TUMBAKU

## Bashe, CCM waingilia kati wakulima tumbaku walipwe

**Na Halima Ikunji,** TABORA

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, amewahakikishia wakulima wa tumbaku kuwa changamoto yao ya kucheleweshewa malipo na wanunuzi wa zao hilo itatatuliwa hivi karibuni.

Akizungumza mjini Tabora mwishoni mwa wiki, waziri huyo alisema kuwa juma hili atakutana na benki za biashara, vyama vya ushirika na bodi ya mazao mjini Dodoma ili kujadili namna ya kukabiliana na tatizo hilo.

Kwa mujibu wa waziri huyo, jumla ya Sh. bilioni 400 zimelipwa kwa wakulima wa tumbaku na hivyo kuhakikishia kuwa malipo yaliyobakia ya bilioni 100 yatalipwa hivi karibuni.

Waziri Bashe alibainisha kuwa jumla ya tani 104,000 kati ya tani 120,000 za tumbaku zimenunuliwa na wanunuzi wa zao hilo.

Hata hivyo, waziri huyo alikiri kuwa baadhi ya wanunuzi wa tumbaku hawajalipa fedha kwa wakulima.

Awali Bodi ya Tumbaku ilisema kuchelewa kwa malipo hayo kunatokana na uhaba wa dola, japo taarifa zinadai kuwa kuna baadhi ya kampuni zinakabiliwa na uhaba wa fedha.

Chanzo hicho kutoka vyama vya ushiriki (AMCOS) tofauti kilimwambia mwandishi jana kuwa kampuni mbili kati ya saba zinazonunua tumbaku, zilishindwa kutimiza wajibu wao wa makubaliano ya kimkataba kwa kuwalipa wakulima kwa wakati.

Sheria na kanuni za sekta ndogo ya tumbaku zinaitaka mamlaka, hususan bodi, kuhakikisha kuwa kampuni zinazonunua tumbaku zina uwezo wa kifedha wa kuwalipa wakulima.

Wiki mbili zilizopita, Kampuni ya Voedsel yenye makao makuu ya Harare, Zimbabwe, ilipewa siku saba na Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Batilda Buriani kulipa Sh. bilioni 20 inazodaiwa na wakulima wa mkoa huo.

Meneja wa Bodi ya Tumbaku Kanda ya Magharibi, Albert Charles, alikaririwa wiki mbili zilizopita akisema bodi imeondoa kampuni hiyo kwenye ratiba ya ununuzi ujao, hadi itakapolipa madeni yote ambayo inadaiwa na wakulima.

Lakini, Meneja wa Kampuni hiyo kikanda, Victor Matawa, aliahidi kuanza kulipa deni lote wiki iliyopita, baada ya kukamilisha utaratibu wa kifedha na Benki ya CRDB.

### KAULI YA CCM

Wakati huo Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani Tabora kimemtaka Waziri wa Kilimo, Bashe) kuhakikisha anafuatilia kwa karibu Kampuni ya Vordsel inayonunua tumbaku mkoani hapa ili iwalipe wakulima fedha wanazodai kwa muda mrefu na kuondoa visingizio vya uhaba wa dola nchini kwa kuwa wakulima hawatambui mambo hayo.

Jana Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Tabora, Hassani Wakasuvi, ambaye ni Mjumbe wa Kamati Kuu Taifa ya chama hicho, alitoa agizo hio wakati wa ufunguzi wa Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani (SUD), akionya kuendelea kuwazungusha wakulima ni kuhujumu nguvu zao.

Alisema amekuwa anapokea malalamiko mengi ya wakulima kutoka Wilaya ya Urambo na sehemu nyingine kuwa hawajalipwa fedha zao toka msimu huu wa ununuzi wa zao hilo. Kufanya hivyo ni kukiuka maagizo ya Rais ya kuwalipa wakulima kwa wakati.

Mkuu wa Wilaya ya Kaliua, Dk. Rashidi Chuachua, akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Tabiora, alikiri kuwapo malalamiko ya wakulima ambao vyama vyao havijalipwa fedha hivyo kumtaka waziri huyo 'kufanya juu' chini wakulima wapate haki yao.

"Hakikisha kampuni inayodaiwa iwalipe haraka ili waendeshe maisha yao na kuzilea familia zao maana malalamiko yamekuwa mengi na majibu hayawaridhishi wakulima," alisisitiza.

Akijibu malalamiko hayo, Waziri Bashe alisema kuwa kutokana na maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan, aliiagiza kampuni hiyo ya ununuzi kuwa mpaka msimu wa tumbaku unapokwisha kila mkulima alipwe fedha zake.


**HALMASHAURI YA WILAYA YA MONDULI**
**SHERIA YA UMILIKISHAJI**
**WA ARDHI YA MWAKA 1999**

**KUPOTEA KWA HATI YA HAKIMILIKI YA KIMILA**

**HATI YA HAKIMILIKI YA KIMILA YENYE USAJILI WA NAMBA 1/MON/66/270**

**MMILIKI ALIOANDIKISHWA:** EPIPHANIA NESTORY KESSY OF P.O. Box 70 MTO WA MBU

**ARDHI:** HATI YA HAKIMILIKI YENYE USAJILI WA NAMBA 1/MON/66/270 WILAYA YA MONDULI.

**MUOMBAJI:** EPIPHANIA NESTORY KESSY OF P.O. Box 70 MTO WA MBU

Taarifa inatolewa kwamba **HATI YA HAKIMILIKI YA KIMILA** iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa **NAKALA HALISI YA HATI YA HAKIMILIKI YA KIMILA** iwapo hakuna pingamizi litakalo tolewa kwa muda wa mwezi mmoja toka tarehe ya taaifa hii itakapotangazwa katika gazeti.

**HATI YA HAKIMILIKI YA KIMILA** ikionekana, irudishwe kwa **MKURUGENZI WA WILAYA-MONDULI S.L.P 01 MONDULI.**

KNY: MKURUGENZI MTENDAJI(W)
MONDULI

RIPOTI YA UCHUNGUZI

# Mjamzito abakwa, afungwa katika kiroba

## -Apewa dawa za kuzuia VVU bila maelekezo, azitupa; maswali yatawala PF3 ilivyojazwa

**Na Mwandishi Wetu,aliyekuwa**
MKURANGA

MJAMZITO amebakwa. Ni usiku wa saa za kulala. Mtoto wake anayeona picha nzima ya mateso kwa mama yake hadi mama anapopoteza fahamu, anachomoka kwenye shuka na kukimbilia nje anakopiga yowe ambalo linawaleta majirani na walinzi wa usiku - sungusungu.

Ni mwezi mzima sasa tangu tukio hili - katika Mtaa wa Kazole, Kata ya Vikindu, kilometa 54.4 kutoka mji wa Mkuranga, mkoani Pwani.

Pamoja na maelezo ya mtoto, mama, majirani, sungusungu na vielelezo kadhaa vinavyoweza kuibua nani wanaweza kuwa wametenda unyama kwa mjamzito, polisi hawajakamata hata mtuhumiwa mmoja.

Mama mwenye umri wa miaka 36 na watoto watatu; ana ujauzito wa miezi sita. Anaishi chumba kimoja na watoto wake na mumewe - dereva wa bodaboda ambaye wakati wa mkewe kubakwa, alikuwa hajatoka kazini.

Ndani ya nyumba hiyo ya vyumba vitano ambayo ujenzi wake haujakamilika, wanaishi pia wapangaji vijana - wanaume wawili wasio na wake wala watoto.

"Ilikuwa Juni 5 mwaka huu, saa nne usiku, nikawa nimegutuka usingizini, huku watoto wangu wakiwa wamelala, nikafungua mlango kwenda msalani nje," anasimulia mjamzito (pichani).

"Niliporudi, nikawa ninachomeka chandarua ila mlango sikuufunga ili kuwe na mwanga humu ndani (nyumba haina umeme) kisha nifunge mlango na kulala. Wakati ninachomeka chandarua, nikakabwa koo kutoka nyuma, nikatupwa chini. Vile ninataka kugeuka niangalie ni nani, nikafunikwa na kufungwa nguo uso mzima."

Mjamzito anasimulia alivyofungwa mikono na miguu pia; "...nikatiwa vidole huku chini" - akionesha sehemu za siri..."

"Ninafikiri aliyenifanyia unyama huu, hakuwa peke yake, maana baada ya kuwa amenidhibiti, walinifunga mikono na miguu kwa kamba.

"Wakiwa wamenifunika uso, mmoja akanikalia eneo la chini ya kitovu. Wakafanya walichotaka..." Ghafla anakumbwa na hisia, anakata masimulizi na kuanza kubugujikwa machozi.

Baada ya robo saa hivi, anapata ujasiri na anaendelea kusimulia: "Baadaye nikakojolewa mdomoni. Pumzi ikaanza kuniishia. Nikawa ninahisi kama ninavalishwa mifuko na kufungwa. Kila nilipojaribu kuita, sauti haitoki, mkojo unaingia mdomoni na puani.

Anaendelea. "Akanyanyuka mtoto wangu wa miaka mitano, alivyokurupuka ndipo wale watu wakatoka. Nilihisi kama walikuwa watu wawili... Mtoto wangu akakimbilia nyumba ya pili na kuita.

"Majirani walivyokuja hapa, walinikuta ninaongea kwa sauti ya chini. Nikapoteza fahamu. Nikaja kuzinduka saa 11 alfajiri nikiwa Hospitali ya Wilaya ya Mkuranga," anaeleza mjamzito.

Anafafanua kwamba mwanawe mdogo aliyechangia kunusurika kwake, alikuwa amelala kwenye kitanda tofauti na mtoto mwenziwe katika chumba hicho.



Mama huyo anasimulia kuwa majirani walioombwa msaada na mtoto, walikuja haraka na kwamba ilikuwa baada ya kuwapa maelezo mafupi kuhusu kilichotokea, alipoteza fahamu.

Kwa mujibu wa mama huyo, kama alivyosimuliwa baadaye, majirani walichukua hatua zote za awali kumpa huduma ya kwanza, kupiga picha za ushahidi na wakati huohuo wakampigia simu mumewe, kumtaka arejee nyumbani kukabili dharura iliyotokea.

Mama mwingine anayeishi jirani na makazi ya mkasa huo ambaye aliomba hifadhi ya jina lake, anajitambulisha kuwa ni miongoni mwa watu wa kwanza kufika eneo la tukio baada ya kufahamishwa na mtoto.

Anataja hatua ya kwanza walipiga yowe lililoitikiwa na umma mwingine kuongezeka, kisha akampigia simu mume wa aliyedhuriwa, huku hatua zingine zikiendelea kuchukuliwa mahali hapo, ikiwamo yeye na mwenzake kupiga picha za ushahidi kwa kutumia simu zao.

Mumewe (jina tunalo) anayejitambulisha kuwa ni dereva bodaboda, hata kipindi cha mkasa huo alikuwa kazini, anamweleza mwandishi namna alivyopokea simu, akitaja muda - saa nne usiku, akiwa njiani anarejea nyumbani kutoka Magomeni, Dar es Salaam.

Anasema alipofika nyumbani, akawakuta Mwenyekiti wa Mtaa na viongozi wenzake, waliompa maelezo kwa kifupi huku akioneshwa picha za ushahidi, ndipo akaungana nao kwa hatua za dharura, wakachukua usafiri wa bajaji kwenda hospitalini, wakianzia Kituo cha Polisi Vikindu.

"Tulianza kwenda Polisi Vikindu, tukapata PF3 (Fomu Na. 3 ya Polisi), ndipo tukaruhusiwa kwenda hospitalini. Alitundikiwa dripu tano za maji, alipopata fahamu ndipo tukaturuhusu kurudi nyumbani.

"Kwenye PF3 hawakuandika chochote, nikairudisha polisi Juni 7 mwaka huu, wakaniambia 'hatuwezi kuipokea kwa sababu haijajazwa chochote'. Niliyoirudisha hospitalini siku iliyofuata (Juni 8, 2023) ndipo wakajaza, na mimi kwa sababu elimu yangu ndogo, sijajua walijaza nini," anasimulia mume, huku akikiri mkewe alipatiwa dawa zikiwamo za kuzuia Virusi vya Ukimwi (VVU) pasipo maelekezo, jambo ambalo mkewe hakukubaliana nalo, akazitupa.

Mwandishi alifika hadi eneo zilikotupwa vidonge hivyo kwenye shamba, umbali wa kilometa moja kutoka nyumba anayoishi mjamzito huyo. Vilikuwa vimenyeshewa mvua.

Kwa mujibu wa mume huyo, walihamia katika makazi hayo Januari mwaka huu, jengo lisilokamilika la vyumba vitano linalomilikiwa na ndugu yao aliyeko ughaibuni, wakitoka Mtoni kwa Azizi Ally wilayani Temeke, Dar es Salaam.

Mwandishi aliporejea kwa aliyedhuriwa kuhusu hisia zake za awali kwa watuhumiwa, hapo moja kwa moja akanyoosha kidole kwa vijana aliowaita 'wavuta bangi' walioishi wote katika jengo hilo.

Anasimulia, kuna wakati walikwaruzana pale alipowataka kwa kile anachokitamka 'wasiishi kihuni' lakini akakutana na majibu 'usituharibie starehe zetu', huku akidai namna walivyoishi na vijana hao ni tishio la moja kwa moja kwa usalama wake na wanawe wawili wadogo wa miaka tisa na mitano, jambo aliloripoti kwa uongozi mtaa. Mtoto wao wa kwanza mwenye umri wa miaka 13 anaishi kwa babu yake mkoani Tanga.

**KIONGOZI WA MTAA**

Boniphace Mtumbuka, Mjumbe wa Shina Na. 3 la Mtaa wa Kazole, anakiri kuwa shuhuda wa mkwaruzano wa zamani katika makazi hayo ulioripotiwa na aliyeathirika, hali kadhalika ni shuhuda wa kilichotokea katika tukio la ukatili dhidi ya mjamzito huyo.

Anasema kuwa baada ya huduma ya kwanza, waliteua mlinzi (sungusungu) na kiongozi mwingine wa mtaa kufuatana na mume na mke aliyedhuriwa kwenda hospitalini.

Anasimulia kuwa muda mfupi baada ya hatua hiyo, mmoja wa vijana wakazi anayeendesha bodaboda, alifika katika nyumba hiyo na udadisi ulipoelekezwa kwake kuhusika na kilichotokea, huku kukiwapo dhamira ya kumkamata, ghafla alitelekeza pikipiki na kukimbia.

Mtumbuka anasema waliamua kuichukua pikipiki hiyo aina ya TVS 125 (namba za usajili tunazihifadhi) kuipeleka Kituo cha Polisi Vikindu, huku nyumba hiyo ikifungwa.

**UFAFANUZI KITABIBU**

Mwandishi alipohitaji ufafanuzi kutoka kwa Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Mkuranga, Shabani Yanda, kuhusu madai ya kutojazwa PF3 na mgonjwa kutofafanuliwa sababu za kupewa vidonge vya kuzuia VVU, aliamuru tabibu mhusika afike ofisini kwake kueleza kilichotokea.

Baada ya nusu saa, daktari mhusika, Seif Mkwinda, alifika na kutoa ufafanuzi kwa mwandishi mbele ya Mganga Mfawidhi kuwa mgonjwa huyo alikuwa amepoteza fahamu na alimfanyia uchunguzi kwa mujibu wa mwongozo wa Wizara ya Afya.

Anautaja mwongozo wa wizara, katika matukio ya aina hiyo, unamtaka tabibu atumie vigezo vitatu: Maelezo ya mgonjwa; kumkagua mgonjwa; na vipimo vya maabara.

Anasema kwa kuwa alikosa maelezo ya mgonjwa aliyekuwa amezirai, akatumia ya mumewe aliyempeleka hospitalini huko.

Dk. Mkwinda anarejea hatua ya pili ya maelekezo hayo aliyotumia, alifuatilia kitaalamu kuthibitisha kuingiliwa kwa nguvu, kupitia michubuko, kuwapo mbegu za kiume na vipimo vya maabara, japo akatoa angalizo maambukizi ya VVU huonekana baada ya mwezi mmoja.

Tabibu huyo anasema uchunguzi ulitoa majibu hasi kuhusu kuambukizwa VVU. Pia hakuona mbegu alipomkagua mgonjwa na baada ya hapo, ndipo akafikia uamuzi wa kitabibu kumlinda kwa dawa za kuzuia VVU, uamuzi unaotokana na kuzingatia maelezo aliyopewa na mume kwamba mkewe alibakwa.

Mwandishi alipohoji sababu za

INAEDELEA UK. 19



Nyumba ulimotendeka ubakaji: **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**

**TANGAZO**

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
## PRESIDENT'S OFFICE - REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
## MUSOMA MUNICIPAL COUNCIL

# FINANCIAL STATEMENT FOR THE FINANCIAL YEAR ENDED 30 JUNE 2022

### FINANCIAL STATEMENT FOR THE FINANCIAL YEAR ENDED 30 JUNE 2022
### STATEMENT OF THE FINANCIAL POSITION AS AT 30 JUNE 2022

| | Note | 2022 TZS | 2021 TZS |
|---|---|---|---|
| **ASSETS** | | | |
| **Current Asset** | | | |
| Cash and Cash Equivalents | 32 | 545,173,437 | 607,597,000 |
| Inventories | 34 | 178,765,113 | 46,017,000 |
| Prepayments | 33P | 457,218,961 | 324,541,000 |
| Receivables | 33 | 7,000,000 | 0 |
| **Total Current Asset** | | 1,188,157,511 | 978,155,000 |
| **Non-Current Asset** | | | |
| Biological Assets | 53 | 0 | 0 |
| Investment Property | 37 | 1,230,923,310 | 1,287,659,000 |
| Other Financial Assets | 36 | 26,744,000 | 26,744,000 |
| Property, Plant and Equipment | 51 | 51,016,398,772 | 59,687,730,000 |
| Work in Progress | 55 | 617,082,618 | 130,000,000 |
| **Total Non-Current Asset** | | 52,891,148,700 | 61,132,133,000 |
| **TOTAL ASSETS** | | 54,079,306,211 | 62,110,288,000 |
| **LIABILITIES** | | | |
| **Current Liabilities** | | | |
| Deferred Income (Revenue) | 46 | 0 | 330,526,000 |
| Deposits | 47 | 100,108,966 | 215,551,000 |
| Payables and Accruals | 39 | 2,475,979,370 | 2,958,139,000 |
| **Total Current Liabilities** | | 2,576,088,336 | 3,504,216,000 |
| **Non-Current Liabilities** | | | |
| Deferred Income (Capital) | 46B | 181,527,492 | 30,020,000 |
| **Total Non-Current Liabilities** | | 181,527,492 | 30,020,000 |
| **TOTAL LIABILITIES** | | 2,757,615,828 | 3,534,236,000 |
| **Net Assets** | | 51,321,690,384 | 58,576,052,000 |
| **NET ASSETS/EQUITY** | | | |
| **Capital Contributed by:** | | | |
| Other Reserves | 104 | 26,744,000 | 26,744,000 |
| Taxpayers/Share Capital | 101 | 0 | 0 |
| **Accumulated Surplus / (Deficit)** | | 51,294,946,384 | 58,549,308,000 |
| **TOTAL NET ASSETS/EQUITY** | | 51,321,690,384 | 58,576,052,000 |

Name : Bosco O.Ndunguru Title: Municipal Director Signature :

Name :William P.Gumbo Title: Municipal Mayor Signature :

Mfumo wa Ulipaji Serikalini (MUSE)

MUSOMA MUNICIPAL COUNCIL — MUNICIPAL DIRECTOR

MUSOMA MUNICIPAL COUNCIL — MAYOR

### FINANCIAL STATEMENT FOR THE FINANCIAL YEAR ENDED 30 JUNE 2022
### CASH FLOW STATEMENT OF THE FINANCIAL POSITION AS AT 30 JUNE 2022

| | 2022 TZS | 2021 TZS |
|---|---|---|
| **CASH FLOW FROM OPERATING ACTIVITIES** | | |
| **RECEIPTS** | | |
| Social Contributions (Revenue) | 236,262,647 | 0 |
| Revenue Grants | 1,382,797,041 | 20,056,861,000 |
| Revenue from Exchange Transactions | 300,000 | 0 |
| Other Revenue | 1,129,388,922 | 977,236,000 |
| Other Receipts | 1,964,250,452 | 0 |
| Levies | 869,715,131 | 305,314,000 |
| Funds Received | 23,324,991,550 | 44,733,000 |
| Fees, fines, penalties and Forfeits | 422,865,813 | 1,343,832,000 |
| **Total Receipts** | 29,330,571,556 | 22,727,976,000 |
| **PAYMENTS** | | |
| Wages, Salaries and Employee Benefits | 18,653,452,509 | 17,107,387,000 |
| Use of Goods and Service | 4,082,805,994 | 2,850,005,000 |
| Social Benefits | 0 | 308,912,000 |
| Other Payments | 2,079,690,101 | 336,774,000 |
| Other Expenses | 129,674,779 | 245,106,000 |
| Maintenance Expenses | 1,176,492,344 | 556,531,000 |
| Grants, Subsidies and other Transfer Payments | 1,012,437,821 | 0 |
| **Total Payments** | 27,134,553,549 | 21,404,715,000 |
| **NET CASH FLOW FROM OPERATING ACTIVITIES** | 2,196,018,007 | 1,323,261,000 |
| **CASH FLOW FROM INVESTING ACTIVITIES** | | |
| **Investing Activities** | | |
| Acquisition of Property, Plant and Equipment | 2,258,441,116 | 1,836,757,000 |
| Acquisition of Biological Assets | 0 | 0 |
| **Total Investing Activities** | 2,258,441,116 | 1,836,757,000 |
| **NET CASH FLOW FROM INVESTING ACTIVITIES** | 2,258,441,116 | 1,836,757,000 |
| **CASH FLOW FROM FINANCING ACTIVITIES** | | |
| **Financing Activities** | | |
| Grants refunded/ transferred | 0 | 0 |
| Borrowing | 0 | 120,000,000 |
| **Total Financing Activities** | 0 | 120,000,000 |
| **NET CASH FLOW FROM FINANCING ACTIVITIES** | 0 | 120,000,000 |
| Net Increase | (62,423,109) | (633,496,000) |
| Cash to be Surrendered to Holding Account | 0 | |
| Cash to be Surrendered to PMG | 0 | |
| Cash and cash equivalent at beginning of period | 607,597,000 | 1,241,093,000 |
| Cash and cash equivalent at end of period | 545,173,891 | 607,597,000 |

Name : Bosco O. Ndunguru Title: Municipal Director Signature :

Name :William P. Gumbo Title: Municipal Mayor Signature

Mfumo wa Ulipaji Serikalini (MUSE)

MUSOMA MUNICIPAL COUNCIL — MUNICIPAL DIRECTOR

MUSOMA MUNICIPAL COUNCIL — MAYOR

### FINANCIAL STATEMENT FOR THE FINANCIAL YEAR ENDED 30 JUNE 2022
### STATEMENT OF THE FINANCIAL PERFOMANCE FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2022

| | Note | 2022 TZS | 2021 TZS |
|---|---|---|---|
| *Classification of Expenses by Nature* | | | |
| **REVENUE** | | | |
| **Revenue** | | | |
| Fees, fines, penalties and Forfeits | 15 | 422,865,813 | 1,343,832,000 |
| Levies | 13B | 869,715,131 | 305,314,000 |
| Other Revenue | 21 | 1,129,388,922 | 977,235,850 |
| Revenue from Exchange Transactions | 17 | 300,000 | 0 |
| Revenue Grants | 16 | 25,246,015,486 | 20,907,905,000 |
| Social Contributions (Revenue) | 20 | 236,262,647 | 0 |
| **Total Revenue** | | 27,904,547,999 | 23,534,286,850 |
| **TOTAL REVENUE** | | 27,904,547,999 | 23,534,286,850 |
| **EXPENSES AND TRANSFERS** | | | |
| **Expenses** | | | |
| Depreciation of Property, Plant and Equipment | 51A | 906,890,115 | 2,204,361,000 |
| Loss on Disposal of Assets | 30 | 9,603,252,546 | 0 |
| Maintenance Expenses | 25 | 1,176,492,344 | 556,531,000 |
| Other Expenses | 28 | 129,674,779 | 245,105,000 |
| Social Benefits | 23 | 0 | 308,912,000 |
| Use of Goods and Service | 24 | 3,675,030,791 | 4,079,774,000 |
| Wages,Salaries and Employee Benefits | 22 | 18,648,979,469 | 17,214,351,000 |
| **Total Expenses** | | 34,140,320,045 | 24,609,034,000 |
| **Transfer** | | | |
| Grants, Subsidies and other Transfer Payments | 26 | 1,018,589,570 | 0 |
| **Total Transfer** | | 1,018,589,570 | 0 |
| **TOTAL EXPENSES AND TRANSFERS** | | 35,158,909,615 | 24,609,034,000 |
| **Surplus / (Deficit)** | | (7,254,361,617) | (1,074,747,150) |

Name : Bosco O.Ndunguru Title: Municipal Director Signature :

Name :William P.Gumbo Title: Municipal Mayor Signature

Mfumo wa Ulipaji Serikalini (MUSE)

MUSOMA MUNICIPAL COUNCIL — MUNICIPAL DIRECTOR

MUSOMA MUNICIPAL COUNCIL — MAYOR

**1.0 INDEPENDENT REPORT OF THE CONTROLLER AND AUDITOR GENERAL**

**Mayor of the Council,**
**Musoma Municipal Council ,**
**P.O. Box 194**
**MUSOMA.**

**1.1 REPORT ON THE AUDIT OF FINANCIAL STATEMENTS**

**Unqualified Opinion**

I have audited the financial statements of Musoma Municipal Council which comprise the statement of financial position as at 30 June 2022, and the statement of financial performance, statement of changes in net assets and cash flow statement and the statement of comparison of budget and actual amounts for the year then ended, as well as the notes to the financial statements, including a summary of significant accounting policies.

In my opinion, the accompanying financial statements present fairly in all material respects, the financial position of Musoma Municipal Council as at 30 June 2022, and its financial performance and its cash flows for the year then ended in accordance with International Public Sector Accounting Standards (IPSAS) Accrual basis of accounting and the manner required by the Local Government Finances Act, Cap. 290.

**Basis for Opinion**

I conducted my audit in accordance with the International Standards of Supreme Audit Institutions (ISSAIs). My responsibilities under those standards are further described in the section below entitled "Responsibilities of the Controller and Auditor General for the Audit of the Financial Statements". I am independent of Musoma Municipal Council in accordance with the International Ethics Standards Board for Accountants' Code of Ethics for Professional Accountants (IESBA Code) together with the National Board of Accountants and Auditors (NBAA) Code of Ethics, and I have fulfilled my other ethical responsibilities in accordance with these requirements.

I believe that the audit evidence I have obtained is sufficient and appropriate to provide a basis for my opinion.

**Key Audit Matters**

Key audit matters are those matters that, in my professional judgment, were of most significance in my audit of the financial statements of the current period. I have determined that there are no key audit matters to communicate in my report.

**Other Information**

Management is responsible for the other information. The other information comprises of Councillors' Report, Statement of Management Responsibility and Declaration by the Head of Finance but does not include the financial statements and my audit report thereon which I obtained prior to the date of this auditor's report.

**Conclusion**

Based on the audit work performed, I state that except for the matters described below, Budget formulation and execution of Musoma Municiapal Council is generally in compliance with the requirements of the Budget Act and other Budget Guidelines.

**(i) Under allocation of own source revenues to development activities 238,912,080**
I noted that, the Council collected total TZS 1,732,027,344.41 net of protected revenues collections during the financial year of which TZS 692,810,937.76 (40%) was supposed to be allocated for implementation of development activities, but only TZS 453,898,858 was allocated. I however found that TZS 238,912,080 out of TZS 692,810,937.76 was not allocated contrary to Para 143 (ii) of the Guideline for Preparation of Government Plans and Budget for 2021/22.

**(ii) Payments for unbudgeted activities worth TZS 169,071,556**
My review of budget implementation documents noted that, the Council implemented 19 activities worth TZS 169,071,556 out of budget contrary to Section 27 (4) of the Budget Act, 2015 and Order 23 (1) of LGFM, 2009 that require very charge of expenditure and items of income to be classified strictly in accordance with the details of the approved budget and the voted funds to be applied only to the purpose for which they were intended.

Charles E. Kichere
**Controller and Auditor General,**
**Dodoma, United Republic of Tanzania.**
**March, 2023**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Klabu, wachezaji kuweni makini kuingia mikataba

**DIRISHA** la usajili Tanzania Bara kwa Klabu za Ligi Kuu, Championship, First League na Ligi Kuu ya Wanawake, limefunguliwa mwishoni mwa juma, Julai Mosi na linatarajiwa kufungwa Agosti 31, mwaka huu.

Kufunguliwa kwa dirisha hilo, kunatoa fursa kwa wachezaji kuhama kutoka klabu moja hadi nyingine kwa wale waliomaliza mikataba yao, waliotemwa kwa makubaliano ya pande mbili, lakini pia kwa klabu kufanya usajili pale inapoona panahitaji kuboreshwa.

Hata hivyo, hiki ni kipindi ambacho kila mchezaji anapaswa kuwa makini zaidi kwa uamuzi atakaochukua wa kusajili katika klabu husika na si kutazama maslahi tu, bali kumulika nafasi yake ya kucheza.

Imekuwa kawaida kwa wachezaji hususan wazawa kuvutiwa kusajiliwa klabu kubwa hapa nchini, Simba, Yanga na hata Azam FC, kutokana na maslahi mazuri, lakini wakajikuta nafasi zao za kucheza ni finyu sana ndani ya msimu mzima.

Baadhi ya nafasi zao za kucheza zimekuwa chini ya asilimia 30 jambo linalowafanya vipaji vyao kushuka na mwisho wa siku kuachwa ama kuishia kutolewa kwa mkopo wakisubiria mikataba yao kumalizika ili kutemwa.

Mbali na hilo, pia katika kipindi hiki tunatamani kuona kila mchezaji kabla ya kusaini mkataba na klabu yeyote anatafuta wataalamu wa sheria/ wanasheria ili kuepusha utata pindi anapotaka kuuvunja hapo baadaye.

Tumelazimika kuyasema hayo mapema kutokana na mvutano unaotokea karibu kila msimu na hivi karibuni katika msimu uliomalizika tukishuhudia Feisal Salum 'Fei Toto' na klabu yake ya Yanga wakiingia katika mzozo kama huo.

Mvutano wao ulihitimishwa baada ya kauli ya Rais wa Jamhuri ya Muungano, Dk. Samia Suluhu Hassan, kuwataka viongozi wa Yanga kutumia busara na kulimaliza suala hilo jambo ambalo lilifanyiwa kazi na Fei Toto kujiunga na Azam FC.


Tunafahamu wachezaji wengi hususan wazawa mara nyingi hutazama fedha za usajili na mshahara tu, huku kilichoandikwa kwenye mkataba huwa hawakijali zaidi ya kusaini, jambo ambalo limekuwa likisababisha mvutano mkubwa wanapotaka kuvunja mikataba yao.

Hivyo, tunaamini kama wachezaji watakuwa na utamaduni wakutumia wanasheria wakati wakuingia mikataba yao, mivutano yote inayosababishwa na uelewa mdogo kisheria ambayo mara nyingine huishia kujitetea kwamba mikataba iliandikwa kwa lugha ya Kiingereza hivyo hawakuielewa vema zaidi ya kusaini, hilo litaepukika.

Lakini pia kwa upande wa klabu tunatambua zipo ambazo zitaingia mikataba na makocha wakigeni pamoja na wachezaji wa nje, nazo hazina budi kuwa makini kwani mara kadhaa tumeshuhudia wanapofika wakati wanahitaji kuivunja huishia kushtakiwa Fifa kutokana na kutofuata utaratibu wa kimkataba. Kwa upande wa wachezaji wa kigeni pia tunakumbuka vema sakata la mshambuliaji wa zamani wa Yanga raia wa Burundi, Hamisi Tambwe, la kuishtaki klabu hiyo Fifa kutokana na madai yake baada ya kuachana, kabla ya kulipwa baada ya shirikisho hilo kuitaka kufanya hivyo la sivyo itaifungia kusajili.

Kwa mantiki hiyo, hatutaki kuona tena klabu na wachezaji wakifikia hatua hiyo hadi kushtakiana Fifa, kwani mbali ya kuzichafua klabu husika, inashusha sifa ya soka letu, hivyo klabu na wachezaji wote hawana budi kuwa makini kwa kutumia wanasheria kabla ya kuingia mikataba.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Mizozo hii kipindi hiki cha usajili haikubaliki abadani

**KWA** miaka mingi kipindi cha usajili Tanzania huwa ndicho cha presha zaidi kwa mashabiki wa soka kuliko hata wakati wa mashindano kama Ligi Kuu, Kombe la FA na michuano ya kimataifa.

Ni kwa sababu ya tabia fulani zisizo za kimichezo na kiungwana kutoka kwa baadhi ya klabu na wachezaji pia.

Kwa wenzetu hiki ni kipindi cha utulivu, mashabiki wanakaa majumbani kwao wakiangalia mitandao ya kijamii, wakisoma magazeti na kusikiliza redio, wakitaka kuangalia mchezaji fulani ametoka kwenye klabu hii na kuhamia nyingine. Ni mchezaji gani amehama huku na kuhamia kule.

Wala hawawazi chochote kingine kama kitatokea, badala yake wanasubiri ligi ianze ili waangalie kama yaliyomo yamo kwa wachezaji waliosajiliwa.

Bongo haipo hivyo, watu wakimaliza msimu wanaingia kwenye ligi nyingine ya usajili.

Kwa bahati mbaya sana hata kamati zetu zinazoshughulikia masuala hayo mara nyingi nazo zimekuwa zikiendeshwa kisiasa zaidi.

Maamuzi yao yanakuwa hayajanyooka, badala yake yanaegemea upande ambao upepo unaelekea.

Kipindi hiki ambacho Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), limefungua dirisha la usajili kwa klabu za Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi ya Championship, Ligi Daraja la Pili 'First League' na Ligi Kuu ya Wanawake msimu wa 2023/24, si ajabu kusikia mchezaji amesajili timu mbili.

Hii ni kawaida kabisa kwenye soka la hapa nchini ambalo kwa kiasi kikubwa limetoka kwenye mfumo wa ridhaa na sasa limekuwa la kulipwa, lakini bado linaonekana kama liko kule kule miaka ya 1960, 1970 hadi 1980.

Ni Bongo tu ndipo mchezaji anachukua pesa klabu mbili wakati mwingine mpaka tatu, halafu kamati inamhalalisha kuchezea klabu fulani, nyingine zikiambiwa kuwa zitarejeshewa pesa zao.

Kanuni hii inawafanya baadhi ya wachezaji kufanya hivyo kwa makusudi, kwani inamfanya asiwajibike kwa lolote au kupata adhabu ambayo inaweza kumfanya kujutia kosa lake na kutothubutu kwake na wengine kurudia tena hata kwa bahati mbaya.

Mchezaji anakusanya pesa klabu mbili, halafu anataka klabu ndiyo ilipe pesa kwa nyingine, huku yeye akiwa ameshakula pesa hizo, huo ni udanganyifu wa hali ya juu.

Kwa bahati mbaya sana moja ya klabu kati ya hizo iwe ndogo dhidi ya kubwa yenye mashabiki wengi ndiyo kabisa, itaonekana ina makosa hata kama itakuwa ya kwanza kumsajili mchezaji husika.

Msimu huu hatuhitaji wachezaji wa aina hiyo, badala yake tunataka wanaojitambua, wanaoamua kusaini mkataba na klabu moja tu, hata kama itakuwa nyingine na kupandisha dau, basi awaambie waende wakazungumze na nyingine, wawarudishie pesa zao, ikiwezekena na pesa ya usumbufu kabla ya yeye kutia wino.

Vinginevyo naishauri kamati itoe adhabu kali kwa wachezaji wa aina hiyo, kwani wanafanya kazi ya kuzigombanisha klabu kwa tamaa zao. Kuna klabu ambazo zinajifanya zina mamlaka juu ya TFF, zinaojiona zina uwezo wa kufanya chochote bila kufanywa lolote.

Hizi nazo zimekuwa zikifanya kipindi hiki kuwa cha wasiwasi, mizozo, kelele na lawama nyingi, watu wakiacha sheria na kanuni zinazoendesha soka na kujikita zaidi kwenye mihemko, siasa na ushabiki.

Klabu hizi zinaweza kumfuata mchezaji ambaye ameshasajili timu fulani, lakini wao wanamuamuru asaini na kwa sababu wana mabavu, watayamaliza tu.

Baada ya hapo unatokea mvutano ambao kwa siasa za mpira wa Tanzania, timu ndogo itashindwa kumpata mchezaji licha ya kuwa ya kwanza kumsajili na kufuata utaratibu wote, huku klabu iliyokiuka taratibu kwa sababu ni kubwa ikipata wafuasi wengi wa kuitetea.

Kwa bahati mbaya sana hata kamati nazo hulalia upande huo huo. Tumeshaona wachezaji wakiidhinishwa kuzichezea timu ambazo zimekiuka utaratibu kwa kumsajili ambaye tayari ameshatia wino sehemu nyingine na wanachofanya ni kuiambia irudishe pesa tu.

Huu ni uonevu na hatutaki kuiona msimu huu. Tunataka kuona kipindi hiki cha usajili wa ligi zote ukienda kwa amani na utulivu, badala ya kuleta mizozo kwenye mitandao ya kijamii na mashabiki kulazimika kupiga kambi ofisi za TFF, kisa usajili.

TANGAZO


A PRODUCT OF
The Coca-Cola Company
KILIMANJARO
DRINKING WATER
FURAHIA MAISHA
NA MAJI ASILIA
500ml
1000ml
1500ml
6L
12L
18.9L
+255 659 536 937, +255 758 979 641, +255 659 785 276
kdw@bbl.co.tz
kilimanjarodrinkingwater
kilimanjaro_drinking_water

# RITA kuzindua mpango usajili watoto wote

**Na Mary Geofrey**

WAKALA wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), unatarajia kuzindua mpango wa usajili wa watoto wote chini ya miaka mitano bure utakaofanyika Uwanja wa Mayunga mkoani Kagera kesho.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa RITA, Frank Kanyusi, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam.

Alisema mpango huo utakaozinduliwa na Waziri wa Sheria na Katiba, Dk. Damas Ndumbaro, unatarajia kusajili watoto 418,246 mkoani humo.

"Mpango huu unalenga kusogeza huduma karibu na wananchi sambamba na kutolewa katika vituo vyote vya tiba vinavyotoa huduma ya afya ya mama na mtoto na ofisi za watendaji kata, hivyo nitoe rai kwa wakazi kujitokeza kwa wingi," alisisitiza Kanyusi.

Alisema maandalizi yote uzinduzi wa mpango huo yamekamilika na kutakuwa na vituo vya usajili 523 na kila kituo kitakuwa na wasajili wasiopungua wawili, waliopatiwa mafunzo maalum ya usajili na utambuzi ili kutimiza majukumu yao kikamilifu.

Alisema utekelezaji wa mpango huo unafanywa na RITA kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ikiwamo serikali ya Canada, Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) na Kampuni ya Simu ya TIGO. Kadhalika, mpango huo utatekelezwa katika awamu mbili, ya kwanza itakuwa kusajili na kutoa vyeti kwa watoto ambao walikuwa hawajasajiliwa na hawana vyeti vya kuzaliwa na ya pili itakuwa kusimika mfumo madhubuti ambao utawezesha kusajili, kutoa vyeti kwa watoto wote watakaozaliwa baada ya mpango huo kuzinduliwa.

"Utekelezaji wa mpango huu ni jitihada za serikali za kuhakikisha kuwa watoto wote wanaozaliwa wanapata vyeti vya kuzaliwa bila kikwazo chochote," alisema.



Mkurugenzi wa Kampuni ya Blue Coast Investment, Athanas Inyasi (kulia) na Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martine Shigella (wa pili kushoto), wakikata utepe kuashiria ufunguzi wa madarasa katika Shule ya Msingi Nyamalembo na Katoma za mjini Geita. Madarasa hayo yamejengwa na Kampuni ya Blue Coast Investment. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Geita, Cornel Magembe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Benki yakabidhi msaada vifaa kwa shule, hospitali

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

BENKI ya CRDB imekabidhi msaada wa vifaa mbalimbali vikiwamo vya shule na hospitali vyenye thamani ya Sh. milioni 30, mkoani Njombe.

Akizungumza wakati wa kukabidhi msaada wa bati 152 kwa Shule ya Sekondari Madilu kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela, Meneja Biashara Kanda ya Nyanda za Juu, Japhary Katura, alisema benki hiyo imeamua kusaidia wilaya tatu za mkoa huo.

"Moja ni kwa Wilaya ya Ludewa ambayo ilikuwa na maombi yanayogusa Shule ya Sekondari Madilu na hapa leo nitakabidhi jumla ya bati 152 na shule shikizi msaada wa bati 152, lakini pia tuliambiwa kuna kituo cha afya zahanati wananchi wanapata shida kubwa wakatuletea baadhi ya vifaa walivyovihitaji na sisi kama benki tumeweza kutoa msaada huo," alisema Katura.

Alisema pia wameigusa Wilaya ya Njombe kwa shule mbili za msingi kwa kutoa madawati 100 na Wilaya ya Wanging'ombe kwa shule ya sekondari wametoa viti 50 na meza 50. "Mkurugenzi wa benki ameniomba nikushukuru na ameniagiza kwa ushirikiano mnaotupa kuanzia ngazi ya kitaifa, ameniambia haitakuwa mwisho bado anaendelea kuangalia maeneo mengine," alisema Katura.

Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Balozi, Dk. Pindi Chana, alisema kuwa msaada huo wa bati utasaidia kukarabati shule hiyo.

"Huu ni mwanzo kwa CRDB na sio mwisho tutakuwa nao pamoja kwa kila hatua," alisema Dk. Pindi.

Mmoja wa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Madilu, Exavery Erick, alishukuru kwa msaada huo wa bati na kuwaomba CRDB kuendelea kutatua changamoto nyingine ambazo zinawakabili ikiwamo kukosekana kwa nishati ya umeme.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
30.06.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **04.07.2023** hadi ***11.07.2023*** kampuni ya **CEVA Interfreight** itasafirisha gari yenye mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka Bandari ya **Dar Es Salaam** kuelekea Mzenga, gari hilo lenye namba za usajili

   **NRB97300 / NRB54202**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

   **Urefu - mita 22.5**
   **Upana - mita 5.40**
   **Kimo - mita 4.70**

3. Njia itakayotumika: Bandari ya **Dar Es Salaam** hadi Mzenga kupitia Barabara ya Mandela, Barabara ya Morogoro gari litasafiri muda wa mchana **( Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni).**

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***


# Maofisa ugani Ruangwa wakabidhiwa

**Na Abdul Mitumba,** RUANGWA

SERIKALI wilayani Ruangwa, imesema itaanza kupima uwezo wa maofisa ugani kwa kuangalia mafanikio katika uzalishaji wa mazao mbalimbali wilayani humo ili kuongeza tija.

Pia imesema haitavumilia maofisa wanaofanyakazi kwa mazoezi badala ya matokeo chanya.

Hayo yamesemwa na Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi (DC), Hassan Ngoma, wakati akikabidhi pikipiki 53 kwa maofisa kilimo ngazi ya vijiji na kata wa halmashauri ya wilaya hiyo.

Pikipiki hizo zilimetolewa na serikali kupitia Wizara ya Kilimo kwa lengo la kuimarisha huduma za ugani ili ziwafikie wakulima kwa wakati hasa wa shambani.

Tukio la makabidhiano hayo lilifanyika katika ghala la kuhifadhia mazao la Lipande nje kidogo ya mji wa Ruangwa na DC Ngoma amewataka maofisa hao kubadili matokeo ya uzalishaji kwa wakulima baada ya kupokea nyenzo hizo.

"Nataka tuwekeane malengo ambayo tutayapima na yapimike kweli. Haiwezekani uzalishaji ukabaki kama ulivyo sasa au kushuka zaidi kipindi ambako hakukuwa na nyenzo kwa wataalamu wetu na sasa ambapo tunawapa pikipiki hizi," alisema.

DC Ngoma alisema anatarajia kuona maofisa kilimo kote wilayani wanasambaa vijijini hasa katika maeneo ya mashamba kuangalia mwenendo wa uzalishaji wa mazao, hasa ikizingatiwa taifa limepitia katika kipindi kigumu cha ukame.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, Andrew Chikongwe, alisema pikipiki hizo zimetolewa ili kuongeza uwezo wa wagani kuwafikia wakulima shambani kwa wakati na kuwashauri namna bora ya kufanya hili kuongeza tija katika uzalishaji.

"Sisi wote hapa tunajua kuwa, kilimo ndiyo uti wa mgongo na kinaajiri watu wengi zaidi kuliko sekta nyingine yoyote, hivyo ni tarajio langu pikipiki hizi zinakuja kuinua uchumi kwa wakulima wetu na wilaya kwa ujumla," alisema.

Mmoja wa maofisa ugani waliopokea pikipiki hizo, Anuari Engema, alisema hatua hiyo ni sawa na ukombozi kwa huduma za ugani kwa wakulima na anaamini uzalishaji utaongezeka kwa kasi.



# Miradi mingi kuwa viporo kwa mpasua kichwa RC

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, amesema uwepo wa miradi mingi ambayo haijakamilishwa kwa muda mrefu katika Halmashauri ya Wilaya ya Karatu, mkoani Arusha, ni mojawapo ya mambo yanayo mpasua kichwa.

Hivyo, amemwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Juma Hokororo kuhakikisha miradi iliyokwama inakamilika, huku akieleza kushangazwa na hali hiyo, licha ya serikali kupeleka fedha.

Alionyesha kutofurahishwa na miradi hiyo mwishoni mwa wiki, alikokwenda kufuatilia hatua walizochukua kuhusu utekelezaji wa hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu na Serikali za Mitaa (LAAC), kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Hivyo, alitoa siku saba kwa Mkurugenzi Mtendaji, kukabidhi gari la Mkuu wa Idara ya Ukaguzi wa Ndani ili watumishi wa idara hiyo waweze kutekeleza majukumu yao kila siku.

Pia aliwasihi madiwani wa halmashauri hiyo kufuatilia miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo yao kwa kina na kamati ya fedha na uongozi kufanya ziara za kukagua miradi kila mara na kutokubali kupitisha fedha za miradi kabla ya kujiridhisha na ujenzi huo.

"Nawaomba acheni mchezo wa kucheza na fedha za miradi ya maendeleo. Haiwezekani mnaletewa fedha sawa na halmashauri nyingine, halafu mnashindwa kukamilisha miradi husika wakati wenzenu wanakamilisha tena ndani ya muda.

"Najua wewe mkurugenzi ni mgeni hapa, lakini simamia miradi kikamilifu lakini madiwani na nyie simamieni miradi inayotekelezwa kwenye maeneo yenu na mkiona kuna tatizo au harufu ya upigaji, toeni taarifa kwa vyombo husika ili hatua zichukuliwe mara moja," alisema.

Kwa mujibu wa Mongella, moja ya miradi ambayo imeshindikana kukamilika licha ya kuletewa fedha na serikali kuu ni miradi wa Kituo cha Afya cha Mbuga Nyekundu, ambacho kilitetewa Sh. milioni 500 lakini mpaka sasa hakijakamilika, licha ya kuongezewa fedha bado milango iliyowekwa kutokidhi mahitaji.

Mongella alitaja miradi mingine isiyokamilika ni pamoja na mradi wa Sequip ambapo fedha zimekwisha na miradi hajakamilika, wakati halmashauri nyingine zilishakamilisha na hadi fedha zimebaki.

"Mkurugenzi (DED), Kituo cha Afya cha Mbunga Nyekundu ni changamoto mpaka sasa zinahitajika Sh. milioni 90 kukamilisha jengo la mama na mtoto na jengo la upasuaji.

"Na hapa mliletewa Sh. milioni 250, lakini mmeshindwa kukamilisha. Nakuagiza tafuteni fedha popote hilo jengo likamilike ili wananchi wapate huduma.

Zaidi aliongeza: "Haiwezekani Rais Samia Suluhu Hassan, anatafuta fedha za kuwaletea wananchi maendeleo halafu watu wachache wanamuhujumu hii sitakubali. "

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Karatu, Dadi Kolimba, alikiri uwepo wa miradi mingi ni viporo na haikamiliki kwa wakati na hali hiyo inatokana na kamati za ujenzi kwenye miradi husika kuongeza bei za vifaa tofauti na bei halisi zilizoko madukani kwa lengo la kujinufaisha.

"Kamati za wananchi zinazoundwa kwenye maeneo ambayo miradi inatekelezwa zinashirikiana na baadhi ya wakuu wa idara kuongeza bei za vifaa na hili nimeshalikemea, ikiwa ni pamoja na kuwaelekeza vifaa vya miradi vinunuliwe moja kwa moja viwandani, ili kupunguza gharama na miradi ikamilike kwa ubora unaotakiwa lakini bado hawatekelezi," alisema.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Karatu, Lucas Kazingo, alikiri kituo hicho cha afya kutokamilika huku akiahidi kuwa wameshanza kutafuta fedha kupitia kwa wadau mbalimbali ili wakamilishe ujenzi wake.

Diwani wa Kata ya Baray kilipo Kituo cha Mbuga Nyekundu, Elitumaini Rweyamamu, alimshukuru Rais Samia kwa kuwaletea Sh.milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya.



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Muheza mkoani Tanga, Dk. Jumaa Mhina (kulia), akiangalia ubora wa machungwa ambayo ni zao la biashara wilayani humo, alitoa hamasa kwa wananchi kuendelea kulima zao hilo kwasababu serikali iko katika hatua za kujenga kiwanda cha kusindika. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Japan kusaidia utatuzi migogoro binadamu, wanyama

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

MKUU wa kundi la wataalamu wa uhifadhi wanyamapori kutoka Japan, Ryoko Nishino, ameahidi kupeleka ujumbe maalum nchi kwake kuwasihi wananchi kuendelea kuchangia na kufadhili miradi ya kukabiliana na migogoro kati ya binadamu na tembo, nchini Tanzania.

Akizungumza na Nipashe jana katika mahojiano maalum kuhusu ujio wao Tanzania, Ryoko, anayefanya kazi na Shirika la Uhifadhi wa Mazingira Duniani na Wanyamapori (WWF Japan) alisema:

"Tumejifunza mengi kuhusiana na migogoro hii ya tembo na binadamu Afrika. Tunakwenda kuwashirikisha wenzetu wa Japan kutafuta fedha za kuendelea kufadhili miradi hii muhimu. Nilipokuja na wenzangu, tumejifunza mengi na sasa tunaporudi Japan, tunakwenda kutafuta fedha za kufadhili miradi ya tembo, kwa kuwashirikisha wenzetu kuchangia ili miradi hii muhimu iwe endelevu.

...Tumekuja kusapoti masuala ya udhibiti wa tembo, kupitia WWF Tanzania. Hawa wenzetu wanatekeleza Mradi wa SOKNOT (Southern Kenya, North Tanzania) na tumeona namna wanavyopambana na migogoro ya tembo na binadamu katika maeneo yanayoathiriwa zaidi na tembo kuanzia mwaka 2022."

WWF Tanzania, inatekeleza mradi mkubwa wa SOKNOT katika mikoa ya Tanga na Kilimanjaro, ambao unalenga zaidi kutafuta suluhu ya kudumu ya migogoro, kati ya tembo na binadamu (HEC) katika ikolojia ya Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi.

Kwa mujibu wa Msimamizi wa Mradi wa SOKNOT Tanzania, ambaye ni mtaalamu mbobezi wa tembo, Prof. Noah Sitati, mradi huo unalenga kupunguza kwa asilimia 40 migogoro hiyo ifikapo mwaka 2025.

Aidha, mradi huo unalenga kulinda na kuhakikisha wanyamapori wanaovuka mipaka na kutembeleana kutoka Kusini mwa Kenya na Kaskazini mwa Tanzania, pia wanaendelea kupita kwenye mapito yao waliyokuwa wanapita zamani.

# Uholanzi yatenga bil.2.4/- kufadhili vyuo vitatu

**Na Mwandishi Wetu,** ARUMERU

SERIKALI ya Uholanzi imetenga zaidi ya Dola za Marekani milioni moja (Sh. bilioni 2.4) kwa ajili ya ufadhili wa mafunzo kwa vyuo vitatu nchini vilivyoko chini ya Baraza la Taifa la Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Sayansi (NACTEVET) ili kuwawezesha Watanzania kujiajiri wenyewe hususani vijana.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Franklin Rwezimula, alitaja miongoni mwa vyuo vitakavyonufaika na ufadhili huo ni Chuo cha Mifugo Tengeru kilichoko mkoani Arusha.

Vingine ni Chuo cha Mifugo Tengeru (TARI), MATI-Uyole na Chuo cha Mahinya kilichoko Wilaya ya Songea, mkoani Ruvuma, ambavyo mbali na kupata mafunzo, pia vyuo vilijengewa Green House (Jumba kitalu) ili kuboresha mazao ya bustani na kuyaongezea mnyororo wa thamani mazao hayo.


Dk. Rwezimula, alikuwa akizungumza na Balozi wa Uholanzi nchini Tanzania, Wiebe de Boer, aliyekwenda kushiriki ufungaji wa mradi wa kuongeza ujuzi na mafunzo ya kujenga uwezo katika sekta ya ndogo ya horticulture.

"Huu mradi umeendeshwa kwa takribani miaka mitatu baada ya Serikali ya Uholanzi kutoa ufadhili kwa vyuo vilivyopo chini ya NACTEVET. Kimsingi mradi huu umeboresha mitaala kuendana na wakati uliopo, kwa maana ya wanaomaliza mafunzo wanakuwa na uwezo wa kujiajiri wenyewe," alisema.

Aidha, alisisitiza kuwa mradi huo ulilenga zaidi kilimo cha matunda na mboga kwa vitendo zaidi tofauti na dhana ya kukaa darasani kujifunza kwa nadharia.

Mwakilishi wa Katibu Mtendaji Baraza la Taifa la Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Ufundi Stadi, Dk. Amani Makota, alisema mafunzo hayo yameviinua vyuo hivyo kwa kuwapatia vifaa vya kufundishia kwa vitendo tofauti na ilivyokuwa awali wakitumia zaidi nadharia na badala ya vitendo.

Akizungumza katika hafla hiyo, Balozi wa Uholanzi nchini, Wiebe de Boer, alisema wanatambua umuhimu wa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Uholanzi, hivyo kwa kutambua umuhimu wa mazao ya bustani waliona ni vyema kutoa ufadhili huo.





# LVBWB yadhibiti uchafuzi mazingira Ziwa Victoria

**Na Vitus Audax,** MWANZA

BODI ya Maji Bonde la Ziwa Victoria (LVBWB), imewahakikishia watumiaji wa Ziwa Victoria kuwa imefanikiwa kudhibiti shughuli za uchafuzi wa ziwa hilo kupitia utiririshaji wa majitaka kutoka viwandani, migodini pamoja na taasisi nyingine zenye uzalishaji wa kiwango kikubwa cha maji taka.

Inaelezwa kuwa kwa sasa hakuna kiwanda wala mgodi wowote ndani na nje ya Kanda ya Ziwa kinachoendesha shughuli za uchafuzi katika ziwa hilo.

kwani zimedhibitiwa kupitia sheria inayozitaka sehemu hizo kutengeneza mabwawa ya kutibu maji taka kisha kupimwa na maabara ya LVBWB kabla ya kuruhusiwa kutiririshwa kwenda katika vyanzo vya maji.

Akizungumza na Nipashe juu ya hali ya uhifadhi wa Ziwa Victoria, Ofisa Uhusiano kwa umma kutoka LVBWB, Mhandisi Gerald Itimbula alisema kwa sasa hakuna kiwanda chochote wala taasisi inayotiririsha maji taka ziwani.

Aliongeza kuwa mpaka maji hayo taka yatibiwe kutokana na takwa la kuweka katika eneo la kiwanda mfumo wa kutibu maji hayo kisha kupimwa na maabara yenye ithibati ya kimataifa ya LVBWB kuhakikisha usalama wake ndani ya ziwa.

"Wapo waliokiuka takwa hilo na sheria ikachukua mkondo wake kwa kuwatoza faini isiyopungua Sh. milioni tatu na isiyozidi Sh.milioni 50 kifungo kisichopungua miaka 12 jela au vyote kwa pamoja sambamba na kugharamia kusafisha uchafuzi uliofanyika," alieleza.

Akieleza jukumu la maabara ya Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Victoria, katika kuhakikisha watumiaji wa chanzo chochote cha maji katika eneo la Bonde la Ziwa Victoria, Mkemia na Meneja wa Maabara hiyo, Frank Balegu, alisema kuwa maji yote yanayotumika yanakuwa salama kwa afya ya binadamu pale tu yanapokuwa yamepimwa na kupataa vibali vya matumizi.

"Baada ya kufanya vipimo sisi kama maabara na kuona kuwa kuna aina yoyote ya uchafuzi, jukumu letu ni kuhakikisha tunadhibiti uchafuzi huo na kuchukua hatua stahiki kuhakikisha hiyo hali inakwisha na haijirudii," alieleza Balegu.

Kadhalika aliongeza kuwa maji yoyote si salama mpaka yapimwe na ili kudhibiti matumizi holela ya maji, bodi hiyo ina jukumu la kutoa vibali vya matumizi ya maji baada ya kujihakikishia kuwa maji hayo ni salama.

Alisema: "Vipimo na vibali hivyo vinatolewa kwa vyanzo vyote vya maji vikiwamo visima, matumizi ya maji kwa ajili ya umwagiliaji, ujenzi, viwandani pamoja na vibali vya umwagaji maji taka baada ya kutibiwa."




Watu wakishuhudia gari lililopata ajali katika Halmashauri ya Msalala, Kijiji cha Nyambula, Kata ya Ngogwa, Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga baada ya gurudumu la mbele kupasuka na kusababisha baadhi ya abiria kujeruhiwa, jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

## Wakulima walia pembejeo kilimo kutofika kwa wakati

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKULIMA wa mazao ya chakula na biashara mkoani Shinyanga, wameiomba serikali kupitia Wakala wa Usambazaji Pembejeo nchini kuhakikisha pembejeo za kilimo zinawafikia kwa wakati, lengo likiwa ni kutokupishana na msimu wa kilimo.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti wakati wa utekelezaji wa mradi wa PETS uliopo chini ya Chama cha Watu Wasioona kwa ufadhili wa Taasisi ya Foundation for Civil Society walisema uzalishaji umekuwa ukishuka kila msimu kutokana na ucheleweshwaji wa pembejeo.

Denis Muwowo ni mmoja wa wakulima hao kutoka Igunda Halmashauri ya Ushetu alisema, kutokupata pembejeo za kilimo kwa wakati kunasababisha wao kushindwa kuzalisha mazao hayo kwa wingi.

Alisema wanapata pembejeo muda wa kupandia na kukuzia umeshakwisha na kupata mavuno kiasi kwa ajili ya familia tu.

Alisema ili kuzalisha kwa tija mawakala wa mbolea ya ruzuku wanatakiwa kuwasogezea mapema mbolea pamoja na pembejeo hizo ili kuwaondolea adha na gharama ya kuzifuata umbari mrefu katika makao makuu ya wilaya, kwani msimu ujao wa mwaka 2023/2024 wanatarajia kuzalisha zaidi kulinganisha na msimu iliyopita.

Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Jeremiah Inegeja, alisema bado kuna tatizo kwa baadhi ya wakulima kuendelea kulima kilimo cha mazoea na kuwataka wabadilike na walime kwa kufuata ushauri wa wataalamu na watumie mbolea kwani ardhi nyingi udongo wake umechoka.

Alisema kila mwaka manispaa hiyo imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa pembejeo za kilimo na kuzigawa bure kwa wakulima vijana wenye uwezo wa kulima hekari tano na kuendelea.

Alisema lengo likiwa ni kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara na wanapoyapata inakuwa mali yao sio ya halmashauri.

Mwenyekiti wa Chama cha Wasioona wa Mkoa wa Shinyanga, Marco Nkanjiwa, aliwataka wajumbe walioteuliwa kushirikiana na maofisa ugani wa kata kutoa elimu ya kulima kisasa, wahakikishe wanawatembelea mara kwa mara na kuandaa taarifa zinazosaidia kutatua kero zao.

# UVCCM yawatolea uvivu vijana wanaobagua kazi

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

UMOJA wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Wilaya ya Kishapu, umewakumbusha vijana wilayani humo kuchangamkia fursa za ajira na vibarua kwenye miradi inayotekelezwa wilayani humo na kuacha tabia za kubagua kazi na kukaa vijiweni kulalamika juu ya ukosefu wa ajira.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mwenyekiti wa UVCCM Wilaya ya Kishapu, Benard Welema, katika wa vvmkutano wa hadhara wa kusikiliza vvkero za vijana wilayani humo na kuzitafutia ufumbuzi.

Alisema katika wilaya hiyo ya Kishapu kuna miradi mingi ya maendeleo ambayo inaendelea kutekelezwa, ukiwamo ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) ambayo inapita baadhi ya maeneo wilayani humo, vvvmradi wa umeme wa jua awamu ya kwanza megawati 50 na kuwataka wachangamkie fursa hizo ili wajikwamua kiuchumi.

"Changamkieni fursa ambazo zinajitokeza mpate ajira na vibarua, mfano katika ajira za udereva ambazo zimetangazwa na halmashauri, nimeangalia vijana wengi waliomba siyo wa hapa Kishapu ni kutoka maeneo mengine acheni kubagua kazi," alisema Welema.

Aidha aliwataka vijana hao kubadilika kitabia, kwamba fedha za mikopo asilimia 10 za halmashauri zikianza kutolewa tena na serikali wazitumie kimaendeleo kwa kufanya uzalishaji na siyo kwenda kuzinywea pombe na muda wa marejesho ukifika wanakimbia na kuitia hasara serikali.

Kadhakila, aliwatoa wasiwasi juu ya kero zote walizoziwasilisha kwenye mkutano huo na kusema kuwa atazifikisha sehemu husika ili zitapate kutafutiwa ufumbuzi.

Nao baadhi ya vijana walioshiriki mkutano huo akiwamo Elisha Elias wakiwasilisha kero zao walisema vijana wengi wilayani humo wamekuwa wakikata tamaa kuchangamkia fursa wakidai kila wakiomba wamekuwa hawapati na kupewa vijana kutoka maeneo mengine.

Naye Michael Mabula, aliwasilisha kilio cha ukosefu wa mikopo ya bodaboda kutoka kwenye taasisivv za kifedha, sababu ikiwa ni masharti magumu ya dhamana, hali ambayo inawafanya kuendelea kutumikishwa na kushindwa kumiliki bodaboda zao wenyewe na kudumaa kimaendeleo.

Hivyo, aliiomba serikali irudishe mikopo ya halmashauri asilimia 10 ambayo hutolewa kwa vijana, ili waweze kukopa bodaboda na kuwasaidia kuwanyanyua kiuchumi kuliko kuendelea kuendesha bodaboda za watu binafsi ambazo kila siku hupandishiwa marejesho na kushindwa kupata pesa za kufanya maendeleo.

Nipashe
Spotika



MAKOCHA WA5 WANAOWEZA KUMRITHI ANCELOTTI MADRID 12 - 13


CECH

# SAJILI 5 ZA UTATA BAINA YA ARSENAL NA CHELSEA

**LONDON, England**

KLABU mbili pinzani za jiji moja la London nchini England, Arsenal na Chelsea mara nyingi hufanya biashara nyingi sana pamoja.

Wakati Kai Havertz alihama kutoka London Magharibi hadi kwa 'Washikabunduki' wiki hii, alikuwa mchezaji wa hivi karibuni zaidi katika safu ndefu ya nyota wa Ligi Kuu England kufanya mabadilishano hayo.

Huku 'The 'Blues' hao pia wakiwa wamevamia Arsenal mara kwa mara, tunaangalia nyuma sajili tano kubwa zilizozua utata kati ya wababe hao wa London, haya sasa...

**#5. William Gallas (Chelsea kwenda Arsenal, 2006)**

William Gallas alikuwa sehemu ya uhamisho wa utata ambao ulimfanya Ashley Cole kwenda Stamford Bridge.

Lilikuwa ni dili ambalo hasira zilikuwa zikitiririka kila upande, huku Chelsea ikidai kuwa beki huyo wa Ufaransa alitishia kujifunga mabao ikiwa angeruhusiwa kuondoka.

Gallas akaendelea kusababisha utata zaidi, baada ya kuondoka Arsenal na kujiunga na Tottenham Hotspur mwaka 2010 na kuwa mwanasoka wa kwanza kuwachezea wapinzani hao watatu wa jiji moja la London.

**#4. Olivier Giroud (Arsenal kwenda Chelsea, 2018)**

Msimu wa sita wa Olivier Giroud pale Emirates ulimshuhudia mshambuliaji huyo akikosa kibali na kutia saini Chelsea katikati mwa kampeni ya 2017-18.

Licha ya kufunga mabao 105 katika mechi 253 alizoichezea Arsenal na kuisaidia kushinda mataji matatu ya FA, hakuwa kipenzi kabisa cha mashabiki wa 'Washikabunduki' hao.

Mshambuliaji huyo alilipiza kisasi alipoifungia Chelsea katika ushindi wa 4-1 dhidi ya Arsenal kwenye fainali ya Ligi ya Europa mwaka 2019.

**#3. David Luiz (Chelsea kwenda Arsenal, 2019)**

Baada ya vipindi viwili Chelsea, ambapo alikuwa na uwezo mkubwa zaidi, David Luiz alihamia Arsenal kwa pauni milioni 8 mwaka 2019.

Katika msimu wake wa kwanza, alitolewa kwa kadi nyekundu dhidi ya klabu yake ya zamani baada ya kusababisha penalti, ambayo ilikuwa sehemu ya mikwaju mitano ambayo aliitoa msimu wa 2019-2020, na kuvunja rekodi ya Ligi Kuu. Hiyo ilimfanya kuwa beki aliyesababisha penalti nyingi zaidi.

Kampeni hiyo ilikamilika kwa Luiz kuisaidia Arsenal kuishinda Chelsea 2-1 katika fainali ya Kombe la FA mwaka 2020.

**#2. Petr Cech (Chelsea kwenda Arsenal, 2015)**

Baada ya kujijengea heshima kama gwiji wa Chelsea na kushinda msururu wa tuzo za ndani na Ulaya, Petr Cech alisaini Arsenal kwa ada ya pauni milioni 10.

Baadhi ya mashabiki wa Blues hawakufurahi vya kutosha na wakatoa vitisho vya kumuua, lakini hilo halikumzuia kipa huyo kushinda 'Golden Glove' katika msimu wake wa kwanza pale Emirates.

Akiwa Arsenal, Cech alijitahidi kuonesha kiwango cha juu na cha ufanisi. Mchezo wake wa mwisho kabla ya kustaafu ulikuwa fainali ya Ligi ya Europa dhidi ya Chelsea mwaka 2019.

**#1. Ashley Cole (Arsenal kwenda Chelsea, 2006)**

Mzozo kuhusu uhamisho wa Cole ulianza mwaka 2005, alipotozwa faini ya pauni 100,000 na Bodi ya Ligi Kuu England baada ya yeye na wakala wake kukutana na maofisa wa Chelsea bila ruhusa kutoka kwa Arsenal.

Alisaini mkataba wa nyongeza wa mwaka mmoja na Arsenal, kabla na hatimaye kuhamia Stamford Bridge mwaka 2006. Ada hiyo ilikuwa pauni milioni tano, huku Gallas akienda upande mwingine kama sehemu ya kubadilishana.

Akiwa ameshinda mataji mawili ya Ligi Kuu Englad na matatu ya FA pale Kaskazini mwa London, Cole alioongeza medali nyingi zaidi kwenye mkusanyiko wake baada ya kuhamia Magharibi mwa London, ikiwa ni pamoja na Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2012.

## ISIKUPITE

LIONEL Messi atatengeneza dola milioni 50 hadi milioni 60 kila mwaka akiwa Inter Miami. Hiyo inajumuisha mshahara, bonasi ya kusaini na usawa katika timu lakini haijumuishi mikataba ya mapato ya Apple na Adidas. Hiyo itamfanya Messi sasa kuwa ndiye mwanamichezo anayelipwa zaidi nchini Marekani.



Extra Time

# MAKOCHA WATANO WANAOWEZA KUMRITHI ANCELOTTI MADRID



Jose Mourinho

**MADRID, Hispania**

ZINEDINE Zidane, Antonio Conte na makocha watano ambao wanaweza kuchukua nafasi ya Carlo Ancelotti katika Klabu ya Real Madrid ikiwa atajiunga na Brazil mwaka 2024, kama ilivyoripotiwa.

Baada ya miezi kadhaa ya uvumi na uchu wa hadharani sana kutoka kwa Shirikisho la Soka la Brazil, Selecao, wanaonekana kumpata Carlo Ancelotti kama kocha wao mpya ajaye.

Kulingana na ripoti, mara tu mkataba wa sasa wa kocha huyo maarufu katika Klabu ya Real Madrid utakapokamilika mwaka 2024, Ancelotti atachukua nafasi hiyo kama kocha mkuu wa kudumu wa Brazil.

Brazil inatafuta kocha mpya baada ya kuwa na wakati mgumu mfululizo kwenye michuano ya Kombe la Dunia kuanzia mwaka 2006 nchini Ujerumani hadi 2022 nchini Qatar.

Kikosi hicho kilichokuwa kinanolewa na kocha Titte kilitolewa kwenye hatua ya robo fainali na Croatia mwaka jana na hivyo kujikuta kikifanya vibaya kwenye mashindano hayo makubwa kwa mara nyingine tena.

Ikumbukwe kwenye michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2006 iliyofanyika nchini Ujerumani ilitolewa na Ufaransa kwenye hatua ya robo fainali.

Kwenye michuano ya mwaka 2010 iliyofanyika nchini Afrika Kusini, Brazil ilitolewa hatua ya robo fainali na Uholanzi.

Mwaka 2014 michuano iliyofanyika kwenye ardhi yake ilimaliza nafasi ya nne, mwaka 2018 iliyofanyika nchini Russia, Brazil ikatolewa kwenye hatua ya robo fainali na Ubelgiji.

Kwa mara ya mwisho Brazil kutwaa taji la dunia ilikuwa mwaka 2002 wakati michuano hiyo ilipoandaliwa kwa ushirikiano wa nchini mbili, Japan na Korea Kusini na tangu hapo haijawa kwenye ubora wake hadi sasa.

Na ikumbukwe kwamba, Brazil ndio bingwa mara nyingi zaidi wa mashindano hayo, kwani wamebeba taji hilo mara tano.

Makala haya inawaangalia makocha watano ambao Real Madrid inaweza kuwangalia ili kuchukua mikoba ya Ancelotti ambaye tayari ameripotiwa kuwa amefikia makubaliano na Seleca hao, twende sasa...

#1. Raul Gonzalez

Akiwa mmoja wa wachezaji wakubwa katika historia ya klabu na pia kocha wa sasa wa kituo cha kulelea vipaji cha Real Madrid, Castilla, Raul Gonzalez ndiye chaguo la ‘kwanza kutoka ndani’ ambalo ‘Los Blancos’ wanaweza kufanya.

Huku Real Madrid hapo awali wakiwa na mafanikio katika kumpandisha cheo kocha kutoka Castilla hadi kuwa kocha mkuu wa kikosi cha kwanza - walipompandisha Zinedine Zidane - hii inaweza kuwa hatua ya busara kufanya ikiwa Ancelotti ataondoka.

**#2. Xabi Alonso**

Gwiji mwingine wa Real Madrid, Xabi Alonso, amevutia sana katika kipindi kifupi cha kazi yake kama kocha hadi sasa.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia la 2010 amefanya kazi nzuri tangu achukue mikoba ya Bayer Leverkusen, kuiondoa klabu hiyo kutoka sehemu za chini kabisa za jedwali la Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, hadi nafasi za kufuzu kwa Ligi ya Europa.

Alonso anaweza kuwa kitu kikubwa kinachofuata katika usimamizi, lakini kuhamia Real Madrid kunaweza kuwa mapema sana.

**#3. Jose Mourinho**

Kocha ambaye anashikilia asilimia tatu ya ushindi katika historia ya Real Madrid, kumwajiri tena Jose Mourinho bila shaka ana sifa zake.

Hata hivyo, je, hisia zake kwenye mchezo ni za juu vya kutosha na uwezo wake wa kuamrisha chumba cha kisasa cha kubadilishia soka ni cha kuvutia kiasi cha kupata kazi kubwa zaidi katika soka kwa mara ya pili? Jibu: Labda sivyo.

**4. Antonio Conte**

Antonio Conte pengine ndiye kocha mwenye hadhi ya juu zaidi sokoni kwa sasa, na ikiwa Real Madrid wanatafuta mpangaji wa muda mfupi ambaye anaweza kushinda La Liga, basi yeye ndiye mtu kamili kwa kazi hiyo.

Rekodi yake nzuri Ulaya inaweza kuwa kigezo cha kudumu kwa Los Blancos hao na anaweza kuwafikisha sehemu fulani.

**5. Zinedine Zidane**

Mara ya mwisho Zidane alipochukua nafasi ya Ancelotti pale Real Madrid, alishinda Ligi ya Mabingwa Ulaya mara tatu mfululizo, na mtindo wake wa usimamizi ulifanya mabadiliko makubwa kwenye vyumba vya kubadilishia nguo.

Hivyo, yeye bado ana DNA nzuri zaidi na Real Madrid, iwapo watamuona ni vema kumrudisha pale kwenye dimba la Santiago Barnabeu, linaweza kuwa jambo la burasa zaidi kwa kikosi hicho.

CV yake ndani ya kikosi hicho ni ya kuvutia, hivyo anaweza kufanya mambo makubwa zaidi akirudi tena hapo.

## Nukuu


“Ni kwa huzuni kubwa kwamba wakati umefika kwangu kutundika viatu vyangu vya kucheza. Kuanzia siku zangu za kwanza Barca, Arsenal, Barca tena, Chelsea, Monaco na Como, nitazithamini zote. Kuanzia kunyanyua Kombe la Dunia, Euro, hadi kushinda kila kitu England na Hispania na karibu mataji yote ya Ulaya, imekuwa safari ambayo sitaisahau kamwe,” **Kiungo wa zamani wa Barcelona na Arsenal, Cesc Fabregas, akitangaza kutundika daluga mwishoni mwa wiki, akiwa na miaka 36.**



“Ningesubiri kupata uzoefu zaidi. Mwaka mwingine ukiwa Ajax ungekufaa. Hupaswi kwenda mahali fulani ili tu kushiriki. Unapaswa kwenda kwenye klabu ambayo utazingatiwa kama kiongozi na mtu muhimu katika timu. Kila mtu katika chumba cha kubadilishia nguo kwenye klabu yako mpya atakutazama na kusema ‘endelea, tuoneshe unachoweza kufanya. Na ikiwa wachezaji wenzako hawahisi kuwa unaweza kuboresha timu, basi wote hawatakuwa upande wako. Utachukuliwa kuwa mvamizi.” **Nguli wa soka wa Uholanzi, Marco van Basten, akimuonya beki wa Ajax, Jurrien Timber, kufikiria uamuzi wake kabla ya kujiunga na Arsenal**



“Mmoja kati ya One of Haaland [Erling], Mbappe [Kylian] ama Vinicius [Junior], atatwaa tuzo ya Ballon d’Or 2023,” **nyota wa zamani wa Barcelona, Patrick Kluivert.**



# WAZAWA WANAOVUMA DIRISHA HILI LA USAJILI



Mkude

**Na Adam Fungamwango**

TAYARI dirisha la usajili na uhamisho wa klabu zote za Ligi Kuu (NBC Premier League), Championship, First League na Ligi Kuu ya Wanawake nchini, limefunguliwa tangu Jumamosi iliyopita.

Kwa mujibu ya Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), litafungwa Agosti 31, hivyo klabu zinachangamka kipindi hiki kwa usajili pamoja na uhamisho pia. Kilichopo sasa ni vita, kwani klabu zinapambana huku na kule kusaka wachezaji wanaoona wataongeza kitu kwenye vikosi vyao.

Kuna klabu tayari zimeshaanza kusajili, huku zingine zikikamilisha uhamisho, zipo pia ambazo kwa sasa zina mazungumzo na wachezaji mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Pamoja na kwamba wachezaji wengi wanaofuatiliwa ni wa nje, lakini kwenye makala haya leo tutawaangalia wa Kitanzania 'wanaotrendi' kwenye usajili mpaka sasa...

**#Kennedy Juma**

Beki wa kati wa Simba, Kenndy Juma, anadaiwa kuwa kwenye hatua za mwisho kujiunga na Singida Fountain Gate kuelekea msimu ujao wa mashindano.

Inadaiwa kuwa mlinzi huyo amewekewa donge nono ili kukamilisha usajili baada ya mkataba wake na Simba kutamatika.

Taarifa zinasema uongozi wa Simba ulipanga kumboreshea mkataba endapo angekubali kusaini, lakini msimamo wake ni kutaka kuondoka na sababu kubwa ni kutaka kupata nafasi kubwa zaidi ya kucheza.

**#George Mpole**

Klabu ya Tabora United (Kitayosce) na Geita Gold zinapambana kuwania saini ya mfungaji bora Ligi Kuu msimu wa 2021/22, George Mpole, ambaye ni straika wa FC Lupopo ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

Mtanzania huyo ambaye kwa sasa yupo nchini kwa upande wake amesema hana tatizo kujiunga na klabu yoyote nchini kama watakwenda kuvunja mkataba wa mwaka mmoja uliobaki nchini DR Congo.

Mpole aliyesema kuwa hakucheza mechi yoyote ya ligi nchini humo tangu asajiliwe na klabu hiyo kutoka Geita Gold kutokana na sababu za kiuchumi na amani, alijiunga na klabu hiyo Desemba mwaka jana kipindi cha dirisha dogo la usajili.

**#Jonas Mkude**

Kiungo aliyeachwa na Simba, Jonas Mkude, taarifa zinaeleza huenda akajiunga na Klabu ya Yanga kwa mkataba wa mwaka mmoja ukiwa na vipengele kibao vya angalizo la kinidhamu, lakini zipo tetesi kuwa Klabu ya Dodoma Jiji nayo imeingiza mguu.

Mkude alikichezea kikosi cha pili cha Simba, kabla ya kupandishwa na kuitumikia kwa miaka 13, amekuwa akihusishwa kujiunga na Yanga, lakini ni kama kumekuwa na mgawanyiko kwa baadhi ya wanachama wakongwe wenye nguvu ndani ya klabu hiyo wakipinga usajili huo.

**#Hassan Dilunga**

Habari zinasema amekamilisha dili la kujiunga na JKT Tanzania iliyopanda daraja msimu huu kama mchezaji huru.

Chanzo kinasema amesaini mkataba wa miaka miwili kwenye klabu hiyo, licha ya dalili zote kuonekana angerejea kwenye klabu yake ya Simba

Zipo tetesi kwamba Simba walimtaka Dilunga asaini mkataba kubaki Simba msimu ujao, lakini tayari alikuwa ameshasaini mapema zaidi JKT Tanzania kwa sababu alikuwa hana uhakika wa asilimia zote kama angeweza kusajiliwa Msimbazi.

#Dickson Ambundo

Hivi karibuni alipewa 'thank you' na Yanga, lakini taarifa zinaeleza yupo kwenye mazungumzo na Singida Fountaine Gate kwa ajili ya kujiunga na klabu hiyo kwa msimu ujao wa mashindano.

Mchezaji huyo wa zamani wa Dodoma Jiji, aliitumikia Yanga kwa misimu miwili, lakini hakuongezwa tena mkataba, baada ya kutamatika msimu huu.

**JE, WAJUA?**



ENDAPO Kipa wa Manchester United, David de Gea, hataongezewa mkataba katika klabu hiyo, Kipa wa Everton, Jordan Pickford, Diogo Costa (FC Porto) na Andre Onana wa Inter Milan, ni makipa watatu wenye uwezo mzuri wa kuziba pengo hilo.



# Wanasiasa waonywa upandikizaji chuki, dini, ukabila suala la bandari

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

WANASIASA wametahadharishwa kutopandikiza chuki za udini, ukabila na kuwagawa Watanzania katika suala la uwekezaji wa Bandari ya Dar es Salaam.

Shekhe wa Mkoa wa Singida, Issa Nassoro, alitoa rai hiyo juzi wakati akizungumza na waumini wa dini ya Kiislamu akisema baadhi ya wanasiasa hawana nia njema na suala la uwekezaji wa bandari kutokana na kuzungumza maneno ambayo yanaashiria kuwagawa Watanzania.

Alisema watu walioanza kupandikiza chuki wafahanu kuwa tangu Tanganyika na Zanzibar zilipoungana na kuunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wananchi wa Zanzibar na Tanzania Bara wamekuwa wamoja na kushirikiana katika mambo mengi.

"Wananchi tusiwape nafasi wanasiasa wanaotaka kutugawa marais wote ukianzia Hayati Mwalimu Julius Nyerere wote wamekuwa wakisisita suala la kudumisha muungano hivyo tusiruhusu suala la bandari likawa chanzo cha kuvuruga muungano wetu," alisema.

Aidha, Nassoro aliwataka wafanyabiashara wasikubali kushawishiwa kwa kuuziwa mali za Waislam kama ambavyo imeanza kujitokeza kwa baadhi ya viongozi kuuza mali kinyemela.

Alisema mfanyabiashara yeyote katika Mkoa wa Singida ambaye atakuwa ameuziwa mali za Waislam kinyemela arudishe fedha kwa waliomuuzia kwa sababu Baraza la Wadhamini la BAKWATA ndio lenye mamlaka ya kuuza mali za Waislam na sio kiongozi yeyote.

Mkataba wa makubaliano ya uendeshaji na uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam ulisainiwa Oktoba 25, mwaka jana baina ya Serikali ya Tanzania na Dubai ili kuendeleza na kuboresha uendeshaji wa miundombinu ya kimkakati ya bandari pamoja na maeneo maalumu ya kiuchumi, maegesho ya utunzaji mizigo na maeneo ya kanda za kibiashara.

Aidha, Juni 10, mwaka huu Bunge lilipitisha azimio kuhusu pendekezo la kuridhiwa kwa mkataba huo kwa lengo la kuanzisha ushirikiano katika uendelezaji wa maeneo ya bandari nchini.

Hata hivyo, kumekuwapo na mvutano kuhusu baadhi ya vipengele kwenye mkataba huo ambapo wadau mbalimbali wamedai kuwa havina tija, huku wengine wakienda mbali kwa kudai kuwa bandari imeuzwa.

Kutokana na hofu hiyo, mara kadhaa serikali kupitia watendaji wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) na hata Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, wamekuwa wakitoa ufafanuzi kuhusu wasiwasi huo.

Hivi karibuni Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alisema kuwa maoni yote yaliyotolewa na wadau mbalimbali yatakwenda kufanyiwa kazi kwa uzito na kwamba hakuna yatakayopuuzwa.



Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Dk. Jim Yonazi, akizindua jukwaa Shirikishi la Mawasiliano ya Kidijitali la Afya Moja na namba ya dharura ya kupokea taarifa za maafa lililofanyika juzi Dodoma. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mikoa yenye chakula yaongoza kwa udumavu

**Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia afya, Dk. Wilson Mahera amesema udumavu kwa watoto bado ni tatizo nchini na mikoa yenye uzalishaji mkubwa wa chakula ndio inayoongoza kwa tatizo hilo.

Pia amesema takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 30 ya watoto wenye umri kuanzia siku sifuli hadi miaka nane wanakabiliwa na tatizo la udumavu wa akili nchini.

Dk. Mahera aliyasema hayo juzi jijini hapa, wakati akifunga mafunzo ya kitaifa ya Sayansi ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto yaliyofanyika jijini hapa.

Alisema kutokana na takwimu hizo serikali imeona ipo haja ya kupambana na hali hiyo ili kuwa na watoto ambao watapata malezi na makuzi bora na kuwa na taifa lenye watu wanaoweza kuzalisha na kujiletea maendeleo.

Aidha, alisema licha ya kuhakikisha watoto wa umri huo wanapatiwa lishe bora pia wanatakiwa kulindwa na kupewa uhuru wa kujieleza na kuwashirikisha katika mambo mbalimbali.

"Wapo wazazi ambao wanadhani malezi ni kuwapiga watoto tu na kuwafanya kuwa wa kueleza badala ya kujieleza, wazazi walezi mnatakiwa kutambua kuwa mtoto anatakia kupewa nafasi ya kujieleza na kueleza na kuondokana na tabia ya kuwapiga watoto viboko badala ya kuwapa uwanja mpana wa kujieleza."

"Watoto msiwafanye kuwa na nidhamu ya uwoga badala yake wapeni uhuru wa kujieleza lakini wazoesheni kula vyakula ambavyo vinawajenga kiakili ikiwamo samaki, nyama, nyama ya kuku au nyama yoyote chakula kiwe nyama halafu vyakula vingine viwe ziada na ugali siyo chakula," alieleza Dk. Mahera.

Kadhalika, alisema serikali imeitaka jamii kuwalea watoto wao katika malezi na makuzi bora kwa kuwapatia lishe bora ili kuwatengenezea mazingira mazuri ya maisha yao ya baadaye na kuwaondoa kwenye hatari ya kupata udumavu wa kimwili, kiakili na kisaikolojia.

# Jamii yatakiwa kukaa mguu sawa kujikinga na maafa

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

KATIBU Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Dk. Jim Yonazi, ameitaka jamii kujiandaa kila wakati ili kujikinga na maafa ambayo yamekuwa yakitokea.

Akizungumza kwenye uzinduzi wa Jukwaa Shirikishi la Mawasiliano ya Kidijitali la Afya Moja jijini hapa, Dk. Yonazi alisema Tanzania imepitia historia ya kukabiliwa na matukio ya maafa yatokanayo na majanga na milipuko ya magonjwa ya binadamu na wanyama. Alisema hivyo ipo haja ya kuwa na mipango ya kitaifa inayoratibiwa vyema kuwezesha kubaini viashiria ili kuzuia maafa.

Aidha, alibainisha kuwa ufuatiliaji wa matukio yanayoathiri afya ya binadamu, wanyama na mazingira unatakiwa kufanyika kwa ufanisi kwa kuzingatia dhana ya mpango mkakati wa Taifa wa afya moja 2022 - 2023.

Yonazi alisema kuwa matukio hayo hutokea bila matarajio na huitaji utambuzi wa mapema na kuchukua hatua za haraka za kukabili.

Hivyo, aliwataka watendaji kujifunza kutoka kwa nchi zilizoendelea katika mifumo ya aina hiyo kwa lengo la kuboresha masuala ya menejimenti ya maafa.

Naye Mkuu wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine, (SUA) Prof. Raphael Chibunda, alisema mradi huo wa kuanzishwa kwa jukwaa shirikishi la kidijitali ulizunduliwa mwaka 2022.

Alisema kuwa kwa kupitia mradi huo shughuli mbalimbali zimetekelezwa ili kuhakikisha kituo hicho kinafanya kazi kama ilivyokusudiwa, kwamba SUA ilitoa vifaa vya TEHAMA vya mradi huo vyenye thamani ya Sh. milioni 42.3.

Awali akitoa taarifa ya mradi huo, Ofisa TEHAMA kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, Alex Ndimbo, alisema mfumo huo pia unaenda kuruhusu wananchi wa kawaida kabisa kutoa taarifa kwa serikali au idara husika moja kwa moja kutoka katika eneo la tukio kupitia namba 190 kwa baadhi ya mitandao ya simu.



## Vijana watakiwa kubuni miradi, kutosubiri kuajiriwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIJANA mkoani Mbeya wameshauriwa kubuni miradi ambayo itawasaidia kujiajiri na kuajiri watu wengine badala ya kuendelea kusubiri kuajiriwa na serikali kwa maelezo kuwa ajira kwa sasa ni chache kuliko idadi ya wanaozihitaji.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (NEC) Taifa anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela, aliyasema hayo juzi alipozungumza na baadhi ya vijana wa chama hicho kuhusu mambo mbalimbali yakiwamo ya uchumi.

Mwaselela alisema zipo fursa mbalimbali za uchumi ambazo vijana wanaweza wakazichangamkia na zikawapatia ajira ya kudumu kuliko kuendelea kutembea na bahasha mitaani wakitafuta ajira.

Alisema kwa Mkoa wa Mbeya baadhi ya fursa ambazo vijana wanaweza kuzichangamkia kuwa ni pamoja na kilimo na ufugaji kwa kuanzisha miradi ya vikundi.

"Mkianzisha miradi ambayo inaeleweka mimi nitakuwa tayari kuwasaidia, nendeni Mbarali mkakodi mashamba mlime mpunga mimi nitawasaidia pale mtakapokuwa mnakwama, nawambia mkijikita huko hamtatamani kuajiriwa," alisema Mwaselela.

Alisema kwa wale ambao wanapata fursa ya kuajiriwa wanatakiwa waajiriwe na wafanye kazi kwa bidi lakini kwa wale ambao wanaona ajira zinakuwa ngumu ni vizuri wakajiajiri.

Alisema kwa sasa serikali imeweka mazingira rafiki ya vijana kujiajiri na kuna mikopo ambayo inatolewa hivyo ni vizuri vijana hao pia wakachangamka ili wanufaike na mazingira hayo na wawe miongoni mwa makundi yanayochangia vizuri pato la taifa.

# Wamiliki mabasi, malori waulalamikia mfumo VTS

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAMILIKI wa mabasi na malori katika baadhi ya mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, wamelalamikia mfumo wa ufuatiliaji wa mwenendo wa magari hayo (VTS) wakidai kuwa unawaongezea gharama za uendeshaji wa vyombo hivyo.

Mfumo huo unaosimamiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA) unalalamikiwa na wamiliki wa magari kuwa kifaa kinachotumika kinauzwa kwa bei kubwa lakini wanatakiwa kukilipia kila mwezi.

Wamiliki wa mabasi na malori kutoka katika mikoa ya Mbeya, Njombe na Songwe walitoa malalamiko hayo mwishoni mwa wiki kwenye kikao baina yao na maofisa wa LATRA.

Kikao hicho kilikuwa na lengo la kusikiliza maoni na ushauri kutoka kwa wamiliki kwa lengo la kuboresha usimamizi wa usafiri na usafirishaji nchini hasa kwa kutumia vyombo hivyo.

Mmoja wa wamiliki wa mabasi, Elisonguo Kelya alisema kifaa kinachofungwa kwenye mabasi wanakinunua kati ya Sh. 380,000 na 400,000 lakini wanatakiwa kukilipia kila mwezi Sh. 20,000 jambo ambalo linawaongezea gharama za uendeshaji.

Vilevile alisema endapo dereva akafanya anayeendesha gari husika akafanya makosa yanayohusiana na mfumo huo, adhabu inakwenda kwa mmiliki wa gari jambo ambalo alisema hawatendewi haki.

"Hizi gharama ni mzigo mkubwa kwetu wamiliki kiasi kwamba wakati mwingine huwa tunaona biashara hii haifai tena, tunatumia gharama kubwa sana kwenye uwekezaji," alisema Kelya.

Christopher Mwambepo ambaye ni miongoni mwa wamiliki wa malori, aliomba LATRA wawauzie vifaa hivyo lakini wasivilipie tena ada ya kila mwezi kwa maelezo kuwa haina maana zaidi ya kuwaumiza.

Alisema hakuna sababu ya kuwatoza ada ya kila mwezi kwa kifaa ambacho tayari wanakuwa wamekinunua kwa gharama kubwa huku akieleza kuwa kwa sasa vifaa hivyo ni lazima mmiliki wa basi ama lori awe nacho.

"Ikiwezekana basi mtugawie bure vifaa hivi halafu mwendelee kututoza hiyo ada ya kila mwezi lakini mnatuuzia halafu mnaanza tena kututoza ada hii siyo sawa kabisa," alisema Mwambepo.

Mkurugenzi Mku wa LATRA, CPA Habibu Suluo alisema mfumo huo ni muhimu kwenye vyombo hivyo kwa maelezo kuwa unasaidia kufuatilia mwenendo wa magari yao popote yanapokuwa.

Alisema mfumo huo pia unawasaidia wamiliki wa magari kusimamia matumizi ya mafuta kwenye vyombo vyao na hivyo akawataka kuhakikisha wanafunga kwa ajili ya faida yao.

"Hatutaki mfumo huu uwe kikwazo kwenye biashara na ndiyo maana tumewaiteni kwa ajili ya kupokea maoni yenu, huu ni mfumo muhimu sana kulingana na teknolojia ya sasa," alisema Suluo.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, aliwataka wamiliki wa mabasi na malori kuacha kuchezea vifaa hivyo vilivyofungwa kwenye magari yao ili viwasaidie kweye ufuatiliaji wa vyombo vyao.




Baadhi ya vijana wakazi wa Mji wa Mbalizi mkoani Mbeya wakisaidiana kusukuma baiskeli yenye mikungu ya ndizi jana wakitokea katika mashamba ya Utengule kuelekea soko la Tarafani. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# H/shauri Kyela yagawa miche bure kwa wakulima

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, imezalisha miche bora 33,000 ya michikichi na kuigawa bure kwa wakulima wilayani humo ikiwa ni sehemu ya mikakati ya kuimarisha kilimo cha zao hilo.

Aidha, halmashauri hiyo imeanzisha mkakati huo ili kukuza kipato cha wananchi na kukabiliana na tatizo la uhaba wa mafuta ya kupikia ambao umekuwa ukilikabili taifa na kusababisha bei ya bidhaa hiyo kuwa ya juu.

Miche hiyo imeandaliwa kwa ushirikiano kati ya halmashauri hiyo na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Nchini (TARI) Naliendele ambayo imekuwa ikisaidia masuala ya utaalamu kwenye uzalishaji wa miche hiyo ili iendane na mazingira.

Akizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa kugawa baadhi ya miche hiyo kwa wakulima, Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Kenneth Izirano, alisema miche iliyoandaliwa inatosha kupandwa kwenye mashamba yenye ukubwa wa ekari 674.2.

"Miche hii itakuwa inapandwa kitaalamu na kwa mujibu wa wataalamu ni kwamba kila ekari moja itakuwa na miche 50, ni miche ambayo inaanza kuzaa mapema na hivyo tunaamini kwamba kipato cha wakulima wetu kitaongezeka na hata pato la halmashauri litakuwa," alisema Izrano.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Katule Kingamkono, alisema lengo la halmashauri yake ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2025 wananchi wawe wamepanda zaidi ya miche 500,000 ya michikichi hiyo kwenye maeneo yao.

Alisema wanaigawa miche hiyo bure ili kuwahamasisha zaidi wananchi kulima kwa maelezo kuwa katika miaka ya karibuni kilimo cha zao hilo kimekuwa kikipuuzwa na baadhi ya wakulima.

Alisema zao hilo ni miongoni mwa ubunifu wa halmashauri kupata vyanzo vipya vya mapato kwa miaka ijayo akisisitiza kuwa itakapoanza kuzaa watakusanya mapato yatokanayo na mauzo.

"Tunaamini kwamba baada ya miaka mitano ijayo michikichi hiii itakuwa inazaa, kwa hiyo wananchi wetu watapata kipato lakini na halmashauri itaongeza mapato kutokana na makusanyo ya ushuru," alisema Kingamkono.

Baadhi ya wakulima walisema miche ya kisasa wanayopewa itawasaidia kuondokana na umasikini kutokana na kuongeza kiwango cha uzalishaji wa zao hilo.

Mmoja wa wakulima hao, Aden Kajela alisema kwenye chikichi wanapata faida kutokana na kila kitu kuwa na soko ambavyo ni mafuta, malighari kwa ajili ya kuzalisha sabuni hasa mbegu pamoja na maganda ambayo yanatumika kutandaza nyumbani ili mkiondoa tope.

Akiwagawia wakulima miche hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Josephine Manase, aliagiza miche hiyo pia kugawiwa kwenye taasisi za umma ili kuongeza tija ya uzalishaji wa zao hilo badala ya kuwagawia wakulima pekee.

Aliagiza miche hiyo kugawiwa pia kwenye shule za msingi na sekondari ili nazo zipande kwa ajili ya kufundishia wanafunzi na kupata kipato kitakachotokana na zao hilo.

Alisisitiza kilimo cha zao hilo kuanza kurithishwa kwa watoto tangu wakiwa wadogo ili wakuwe wakijua namna ya kuzalisha na manufaa yake.



## Vijana watakiwa kuchangamkia fursa za mikopo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mtendaji wa Baraza la Vijana Zanzibar, Salum Issa Ameir, amewataka viongozi wa mabaraza ya vijana kuchangamkia fursa za mikopo inayotolewa na Serikali ya Zanzibar kwa lengo la kujiajiri.

Aliyasema hayo jana Zanzibar wakati akizungumza na wenyeviti wa vikundi vinavyojihusisha na uvuvi na utalii vinavyosimamiwa na Baraza la Vijana Zanzibar kutoka shehia mbalimbali za Unguja watakaopatiwa mkopo wa boti za uvuvi unaotolewa na Benki ya CRDB.

Katibu huyo alisema lengo la serekali ni kutoa ajira 300,000 kwa vijana ambapo ajira hizo zitafikiwa kwa kujiajiri, kuajiriwa katika sekta binafsi na chache ndani ya serikali.

Hata hivyo aliwataka viongozi hao kutoa hamasa kwa vijana wingine kuacha kukaa mitaani na kujihusisha na vitendo viovu badala yake kujiunga na vikundi vya ushirika na kuanzisha shughuli mbambali ikiwa ni pamoja na kilimo, uvuvi, ufugaji na utalii.

Viongozi hao wa mabaraza ya vijana waliishukuru serikali kwa kuwaona vijana na kuwapatia mikopo ya fedha na vifaa vitakavyowasaidia kujiajiri na kujikimu kimaisha.

Aidha, viongozi hao wameutaka uongozi wa Baraza la Vijana Zanzibar kuwatetea vijana wazawa kupewa ajira za muda mfupi katika miradi ya ujenzi mbalimbali inayoendelea katika visiwa vya Unguja na Pemba.

Baraza la Vijana Zanzibar linatarajia kutoa boti 64 kwa vikundi vya ushirika vya shehia mbalimbali za Zanzibar.

# DK. Mwinyi aonyesha mwanga wawekezaji Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema atawasaidia wawekezaji wanaokumbana na vikwazo na changamoto mbalimbali ili kufanya biashara zao nchini.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo wakati akizungumza na wawekezaji wa kampuni mbalimbali kutoka China waliofika kuzungumza naye kuhusiana na fursa za uwekezaji zinazopatikana Tanzania.

Akizungumza na mwenyekiti wa kundi la kampuni za Liyu Group, Yuefeng Wang anayejishughulisha na utengenezaji viatu na kuzalisha umeme, alisema nishati kwa sasa inahitajika zaidi Zanzibar kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya viwanda.

Kuhusu biashara ya viatu, Dk. Mwinyi aliwashauri wawekezaji hao kuangalia soko pana la Afrika ili kuuza bidhaa hizo.

Aidha Dk. Mwinyi alikutana na Quan Chen wa kampuni iliyopo Tanzania, iitwayo Tanzania Binjiang inyoshughulika na usindikaji wa nyama.

Pia Dk. Mwinyi alikutana na Xiaoli Zhou mwekezaji wa utalii wa michezo na akamkaribisha kuwekeza Zanzibar, pia pamoja na mambo mengineyo aliwakaribisha kundi la wafanyabiashara wanawake kuitembelea Zanzibar.

Kadhalika, Dk. Mwinyi alifanya mahojiano na vituo viwili vikubwa vya habari vya China vinavyorusha matangazo kwa lugha ya Kiingereza ambavyo ni China Global TV Network na Shirika la Habari la China-XINHUA.

Mahojiano hayo yalijikita zaidi juu ya uhusiano wa China na Tanzania kwa ujumla na sera za China barani Afrika.

Rais Dk. Mwinyi alikamilisha ziara aliyoifanya China aliyoianza Juni 27, mwaka huu.




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akiwa na mkewe Mama Mariam Mwinyi wakiwasili Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume jana kutokea nchini China baada ya kumaliza ziara yake ya kikazi. **PICHA: IKULU**

# SMZ, SJMT kushirikiana kulinda rasilimali za asili

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema itaendeleza ushirikiano na Serikali ya Jamhuri ya Muungano katika mambo ya maendeleo ikiwamo kufanya doria upande wa rasilimali za asili.

Hayo yalisemwa jana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Umwagiliaji na Mifugo, Seif Shaaban Mwinyi, wakati akizungumza na kikosi kazi cha kupambana na biashara ya usafirishaji wa rasilimali za misitu katika ukanda wa Bahari ya Hindi.

Kikao hicho kilihusu maofisa kutoka Wizara ya Kilimo Zanzibar na Wizara ya Maliasili na Utalii ya Tanzania Bara kikao hicho kimefanyika Maruhubi visiwani humo.

Alisema kuwapo kwa ushirikiano katika wizara hizo kutaongeza ubunifu wa kufanya kazi ili rasilimali za misitu kubaki salama.

Alisema kuwapo kwa kikosi kazi hicho cha doria cha pamoja kinaenda kuondosha changamoto na kuwabaini wahalifu hasa wizi wa rasilimali hizo katika ukanda huo.

Alisema hivi sasa Wizara ya Kilimo inachangia asilimia 25 ya pato la taifa katika uchumi wa Zanzibar hivyo kuwapo kwa kikosi hicho cha doria kinaenda kuzidisha mafanikio ya asimilia hizo.

Katibu mkuu huyo alisema kikosi kazi hicho ni jumuishi, kimekusanya wataalamu mbalimbali siyo tu kwa upande wa wizara mbili pia kina wajumbe kutoka vikosi vya ulinzi na usalama Tanzania Bara na Zanzibar.

Alisema kuna changamoto kubwa ya kuibiwa kwa rasilimali za misitu na rasilimali nyingine za baharini kwa vile hakukuwa na doria ya pamoja lakini hivi sasa changamoto hiyo itaondoka.

“Ripoti ya kikosi hiki itakapotolewa itajulikana kazi ya kufanya na kwa vile kikosi hiki cha doro kitakuwa cha kudumu kitaoa mapendelezo katika kuboresha na kuona changamoto walizokumbana nazo,” alisema Mwinyi.

Naye Msimamizi Mkuu wa kikosi hicho, Emmanuel Msofe, alisema kikosi hicho kimeundwa kutokana na maadhimio ya kikao kwa Waziri wa Maliasili na Utalii Tanzania Bara na Waziri wa Kilimo Zanzibar Desemba mwaka jana.

Alisema lengo la kuundwa kwa kikosi kazi hicho ni kupambana na wizi na uharibifu wa biashara ya usafirishaji wa rasilimali za misitu.

# DAWASA kuunganisha wakazi M'nyamala mfumo majitaka

Na Joseph Mwendapole

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DAWASA), imewataka wananchi kuomba kuunganishwa kwenye mfumo wa majitaka ili waondokane na vyoo vya shimo.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na msimamizi wa mradi wa uboreshaji usafi wa mazingira Mwananyamala, uliotekelezwa na DAWASA, Gabriel Wanzagi.

Alisema mradi umekamilika kwa asilimia 100 na kazi iliyokuwa imebaki ya kuunganisha chemba za ukusanyaji majitaka kwa sasa imekamilika.

"Mradi huu umekamilika na ulihusisha kazi ya kuunganisha chemba zote 32. Tunatoa wito kwa wananchi wajitokeze kwa wingi kuunganishwa na mfumo wa majitaka na kuondokana na matumizi ya mashimo ya vyoo," alisema Wanzagi.

Mhandisi Wanzagi aliongeza kuwa mradi huo ni muhimu kwa eneo la Mwananyamala na maeneo jirani na inaenda kusaidia kumaliza kero ya majitaka yaliyokuwa yanatiririka mtaani na kuchafua mazingira.

Mkazi wa Mtaa wa Mwananyamala Kanisani, Hafsa Maulid, alisema amefurahishwa na kukamilika kwa mradi huo ambao alisema unaleta matumaini ya usafi wa mazingira na kuondokana na athari ya milipuko ya magonjwa.

"Mradi huu ni tiba ya tatizo la milipuko ya magonjwa hasa kipindupindu na magonjwa ya kuhara unaosababishwa na utiririshaji majitaka ovyo mtaani, tuna imani kubwa kwamba kukamilika kwake kutasaidia kuyaweka mazingira yetu katika hali ya usafi," alisema.

Alisema mradi huo uliogharimu Sh. milioni 230 umehusisha ulazaji wa bomba za kusafirisha majitaka kwa umbali wa kilomita 1.6, ujenzi wa chemba tatu za kukusanya majitaka na unatarajiwa kuhudumia kaya zaidi ya 100.

Alitaja mitaa itakayonufaika na mradi huo kuwa ni Msufini, Barabara ya Dunga, Mwananyamala Kanisani na maeneo jirani.

Hivi karibuni Kampuni ya ujenzi ya Metito ya Misri, ilisaini mkataba wa kusanifu, kujenga na kuendesha mtambo mpya wa kuchakata majitaka katika eneo la Mbezi Beach, mkoani Dar es Salaam. Tanzania mradi unaotekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali na Benki ya Dunia (WB).

Mradi huo unaotekelezwa na Serikali ya Tanzania kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), unatarajiwa kuchangia katika kuboresha usafi wa mazingira kwa kuwezesha majitaka kukusanywa na kutibiwa kikamilifu.



Mhifadhi Mkuu wa Hifadhi ya Mikumi mkoani Morogoro, Kamishna Mwandamizi Msaidizi wa Uhifadhi, Ignas Gara (kulia), akizungumza na baadhi ya wafanyakazi wa Wizara ya Maliasili na Utalii walipotembelea hifadhi hiyo mwishoni mwa wiki kwa ufadhili wa Mradi wa Kuboresha Usimamizi wa Maliasili na Kukuza Utalii Kusini mwa Tanzania (REGROW). **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Watakaokwamisha ujenzi miundombinu shule kukiona

Na James Mwanamyoto

NAIBU Katibu Mkuu (Elimu), Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Dk. Charles Msonde, amesema serikali haitomsamehe mtu yeyote atakayebainika kukwamisha ujenzi wa miundombinu ya elimu katika shule za sekondari na msingi.

Dk. Msonde alisema hayo kwa nyakati tofauti wilayani Msalala, Ushetu na Kahama Manispaa, kukagua utekelezaji wa ujenzi wa miradi ya miundombinu ya shule za msingi na sekondari katika halmashauri hizo.

"Serikali haitomsahe yeyote atakayesababisha wanafunzi wakose mabweni na madarasa wakati imetoa kwa wakati fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hiyo ya elimu," alisisitiza Dk. Msonde.

Ili kuhakikisha miundombinu ya elimu inakamilika kwa wakati, Dk. Msonde alizitaka menejimenti za halmashauri hizo kuongeza mafundi wenye uwezo wa kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya elimu katika shule za sekondari na msingi ili wanafunzi wapate mazingira bora ya kupata elimu.

Aliongeza kuwa, ujenzi wa miundombinu hiyo ya elimu kupitia mradi wa Boost ilikuwa imepewa muda maalumu wa kukamilika na kuwataka viongozi wa halmashauri zote nchini ndani ya siku 10 wanakamilisha miundombinu hiyo ili iweze kutumiwa na wanafunzi.

Kaimu Katibu Tawala, Mkoa wa Shinyanga ambaye ni Ofisa Elimu Mkoa wa Shinyanga, Dafroza Ndalichako amesema, ofisi yake itahakikisha watendaji wa halmashauri zote zinazotekeleza mradi wa Boost katika eneo lake la utawala, wanafanya kazi usiku na mchana ili kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya elimu.

## Wananchi wahamasishwa kujenga tabia ya kutembelea hifadhi

Na Ibrahim Joseph, MOROGORO

WANANCHI na wafanyakazi wa sekta mbalimbali wametakiwa kujenga tabia ya kutembelea vivutio vya utalii vilivyopo kwenye hifadhi za hapa nchini.

Mhifadhi Mkuu wa Hifadhi ya Mikumi, Kamishna Mwandamizi Msaidizi wa Uhifadhi, Ignas Gara, alitoa kauli hiyo wakati alipozungumza na baadhi ya watumishi wa Wizara ya Maliasili na Utalii walipotembelea hifadhi hiyo mwishoni mwa wiki.

Gara alisema wafanyakazi hao na wananchi wanatakiwa kujenga tabia ya kupenda kutembelea vivutio vya utalii vilivyopo kwenye hifadhi mbalimbali za nchini.

"Nawashukuru watumishi wa wizara yetu kwa kufika kutembelea hifadhi yetu, karibuni sana nawapongeza kwa uamuzi huu wa kuthubutu kufanya utalii huu wa ndani," alisema Gara.

Alisema vivutio hivyo ni mali yao na wanatakiwa kuvitembelea na kujifunza mambo mengi yaliyopo kwenye maeneo hayo ya uhifadhi.

Kadhalika, alisema kuna maeneo mengi yenye vivutio vizuri na wananchi kupitia vikundi, Taasisi na mtu mmoja mmoja wanakaribishwa kutembelea.

Alisema mfano wa hifadhi yao inafikika kwa urahisi kwa kuwa kuna barabara kuu ya kutoka Morogoro kwenda Iringa.

Kadhalika, gharama za kuingia hifadhi na kufanya utalii ni rahisi, kwa Watanzania wanalipa chini ya Sh. 6,000 kwa siku na watoto chini ya miaka mitano hawatozwi gharama za kuingia hifadhini.

Aliwataka baadhi ya wananchi kuondoa mawazo ya kufikiri kuwa wanaotakiwa kwenda kutalii kwenye hifadhi ni wageni kutoka nje ya nchi.

Alisema kwa wasiokuwa na usafiri watalazimika kukodisha magari kwa watoa huduma za usafiri waliopo maeno mbalimbali nchini.

Kamishna Igara alisema, hifadhi yao inaruhusu watu binafsi kutumia chombo chao cha usafiri wowote kuingia kuzunguka ndani kuangalia vivutio vilivyopo baada ya kulipia.

Aidha, alisema idadi ya watalii wa nje imekuwa ikiongezeka kila mwaka kutokana na uwanja wa ndege ndani ya hifadhi.

Kiongozi wa msafara wa wafanyakazi wa wizara hiyo, Adrianet Kibabage, alisema ziara yao imefadhiliwa na Mradi wa Kuboresha Usimamizi wa Maliasili na Kukuza Utalii Kusini mwa Tanzania (REGROW).

Kibabage alisema kuna jumla ya wafanyakazi 17 kutoka idara ya utunzaji kumbukumbu na nyaraka, wasaidizi wa ofisi na makatibu muhtasi, watakuwa na ziara ya kutembelea Hifadhi ya Mikumi na Hifadhi za Mlima wa Udzungwa.

Aliushukuru mradi kwa ufadhili uliowawezesha kutembelea vivutio vilivyopo kusini mwa nchi na watu wengine miongoni mwao walikuwa hawajawahi kufika maeneo hayo.

# Mjamzito abakwa, afungwa katika kiroba

**INATOKA UK. 4**



Mume na mtoto wakionesha eneo ambalo mjamzito alitupa dawa alizopewa hospitalini Mkuranga.

mgonjwa kupewa dawa za kuzuia VVU bila maelekezo, pia kutojazwa PF3, daktari huyo akajitetea:

"Mimi nilikwenda mpaka kitengo kinachotoa dawa hizi. Kitengo kilimtembelea, wakajiridhisha kama yupo timamu na alipewa elimu ya athari zake kwa sababu hizo ni dawa za kutumia kwa muda mrefu -mwezi mmoja.

"Sasa, kama alizitupa, hiyo ni changamoto ya mtu aliyempa dawa. Lakini kama aliona hajapewa maelekezo, si angerudi kutoa taarifa!

"Kuhusu kujaza PF3, utaratibiuu wa wizara - mtu aliyempokea mgonjwa ndiye anatakiwa amjazie lakini mimi wakati ninaondoka hospitalini, (mjamzito) alikuwa amepoteza fahamu. Asubuhi alipozinduka alielekezwa aje siku nyingine, atanikuta na alipokuja siku hiyo nilimjazia na akaondoka nayo."

**MGANGA MKUU**

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Dk. Gunini Kamba, anaeleza utaratibu unaotumika kwa mgonjwa aliyebakwa, anatakiwa kuwahi hospitalini na asijisafishe, ili kuwasaidia madaktari kufanya uchunguzi kwa kuchukua sampuli zitakazoonekana.

Kuhusu ujazaji wa PF3, Dk. Kamba anasema inaendana na namna tabibu anavyomwona mgonjwa, ikimwongoza kujaza kile kitakachoisaidia polisi na kwamba ujazaji huo unapaswa kufanyika kuanzia siku ya kwanza.

Anafafanua kuwa pale mgonjwa anapoendelea na matibabu, ujazaji PF3 nao unakuwa endelevu, hivyo mgonjwa kuondoka hospitalini bila kujazwa PF3 si sahihi. Anabainisha kuwa dosari hiyo mara nyingi ni zao la uelewa duni wa baadhi ya matabibu katika hatua hiyo.

"PF3 itaendelea kujazwa kwa wakati unaostahili lakini siku ya kwanza lazima ijazwe jinsi mgonjwa alivyoonekana kabla hajapata matibabu na baada ya matibabu, ni kitu ambacho ni endelevu," alisisitiza.

Kwa mujibu wa Mganga Mkuu wa Mkoa, inapaswa mgonjwa aliyepitia polisi kuchukua PF3 afike hospitalini, mpelelezi akiwa mmoja wa wanaomsindikiza.

Hivyo, kufuatia utata unaotokana na ujazaji wa PF3 hospitalini Mkuranga, Dk. Kamba anasema analifuatilia suala hilo na ikiwezekana ataunda timu ya kuchunguza ukweli wake.

Ni hoja ambayo mwanadishi alipowasiliana na Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, Dk. Anna Henga, aliiungana na msimamo wa Mganga Mkuu wa Mkoa uchunguzi ufanyike.

Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Dk. Rose Reuben, pia anaunga mkono uchunguzi ufanyike, akitaka Jeshi la Polisi lichukue hatua dhidi ya wahusika wa unyama dhidi ya mjamzito.

"Tunalaani kitendo hiki, hawajamfanyia mama pekee, bali pia mtoto aliyeko tumboni. Kwa desturi zetu na mila za kitanzania, mama mjamzito anapaswa kuenziwa, kuheshimiwa, kupewa usaidizi wa karibu wa upendo kwa sababu analeta kiumbe kipya duniani. Analeta Taifa la kesho.

"Kiumbe hicho kinapaswa kuwa na akili timamu na umbo timamu. Mama apofanyiwa ukatili wa namna hiyo, kiumbe kitatoka kikiwa na upungufu. Sisi watetezi wa haki za watoto, wasichana na wanawake tunalaani vikali kitendo hicho. Wahusika wakamatwe na kufikishwa mahakamani," anasema Rose.

**RPC RUFIJI**

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Rufiji, Kamishna Msaidizi Kanuti Msaki, anakiri kuwa na taarifa za tukio hilo zilizoripotiwa Kituo cha Polisi Vikindu Juni 5 mwaka huu.

"Huyo mtu (mlalamikaji) ni kweli inadaiwa alibakwa na pikipiki ilifikishwa kituoni. Mtuhumiwa bado tunaendelea kumtafuta. Mtu wetu anayeshughulika na dawati la jinsia ameshakwenda mpaka nyumbani kwa mhusika, akachukua maelezo yake ambayo kwa sasa yapo kituoni pamoja na kielelezo cha pikipiki," anasema.

Kamanda Msaki anataja kinachoendelea kwa sasa ni kumsaka mtuhumiwa. Jeshi limeishirikisha Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kubaini mmiliki wa pikipiki iliyoko polisi.

"Tunafuatilia TRA kujua mmiliki wa pikipiki ni huyo anayedaiwa kufanya kitendo hicho au ni dereva tu au kama ni mtu mwingine," anafafanua.

Wakili wa Kujitegemea, Hamisi Mayombo, akizungumzia ukatili uliofanywa dhidi ya mama huyo, anarejea Kifungu cha 130(1) cha Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16, kinachotamka: "Ni kosa kwa mtu wa jinsia ya kiume kumbaka msichana au mwanamke."

Wakili Mayombo pia anarejea kifungu cha 131(1) cha sheria hiyo kinachoelekeza adhabu ya kifungo cha maisha gerezani kwa mtu anayetenda kosa la kubaka, ikiambatana na adhabu ya viboko na faini, na atatakiwa kulipa fidia ya kiasi ambacho kitatamkwa na mahakama, kwa mtu ambaye ametendewa kosa hilo na kwa majeraha aliyoyapata.

Kimsingi, ukatili dhidi ya mjamzito huyo unakinzana na Ibara ya 16(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, inayoelekeza "kila mtu anastahili kuheshimiwa na kupata hifadhi kwa nafsi yake, maisha yake binafsi na familia yake na unyumba wake, na pia heshima na hifadhi ya maskani yake na mawasiliano yake ya binafsi."

Ibara hiyo ya Katiba ya nchi pia inataka serikali kuweka utaratibu wa sheria kulinda haki ya mtu ya faragha na ya usalama na nafsi yake, mali yake na maskani yake.

Vilevile, uhalifu uliofanywa dhidi ya mjamzito huyo, unakinzana na Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia Tanzania ya Mwaka 2000 inayolenga kuweka mazingira wezeshi, kutatua vikwazo dhidi ya wanawake na kuleta haki na usawa ili kundi hilo lishiriki kikamilifu na kwa ufanisi katika programu na miradi ya maendeleo.

Kitendo hicho pia kinakwaza utekelezaji wa Lengo Na. 5 la Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG) linalozitaka nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa (UN) kuhakikisha zinatilia mkazo usawa wa kijinsia.

Tanzania pia imeshatia saini na kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW) wa Mwaka 1979, unaoelekeza kuondoa aina zote za ubaguzi na uonevu kwa wanawake.

# PSSSF yahadharisha wastaafu dhidi utapeli

**Na Beatrice Shayo**

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), umewatahadharisha wanachama wao wastaafu kuwa makini na utapeli mpya uliojitikeza na kusababisha baadhi yao kuibiwa fedha zao kwenye akaunti bila wao kujijua.

Kadhalika, PSSSF imesema hali ya mfuko ipo vizuri na thamani ya fedha ni Sh. trilioni 8.3 ambao una uwezo wa kuwalipa wastaafu bila ucheleweshaji.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Meneja Uhusiano na Elimu kwa Wanachama, Mfuko wa PSSSF, James Mlowe, wakati akizungumza na waandishi wa habari katika maonyesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa yanayoendelea kwenye Viwanja vya Mwalimu Nyerere.

Alisema matapeli hao kwa sasa wamekuja na utapeli mpya baada ya kuona ule wa zamani umegonga mwamba kwa kutuma ujumbe mfupi kwa baadhi ya wastaafu kuonyesha kuwa akaunti yao imefungiwa.

"Maana yake ukienda benki huwezi kupata fedha sasa wanajifanya wanatoa solution (ufumbuzi) namna ya kufungua akaunti yako ili uendelee kupata fedha ukiendelea kuwapa maelekezo ya kutuma ujumbe kwenye namba ambayo wanakutumia kwa haraka haraka unaweza kujua kama ni namba ya simu mstaafu ukituma maelezo yake ndiyo wanapata uhalali wa kutoa fedha kwenye akaunti yako," alisema Mlowe.

Alisema ni vizuri mtu anapopata ujumbe kwenye simu yake utoe taarifa kwa mfuko wa PSSSF ili kuepuka kutapeliwa kutokana na tatizo hilo kuwa kubwa kwa wastaafu kutapeliwa.

Alisema wapo wanaotoa taarifa ya kutapeliwa na wengine hawatoi baada ya kugundua ametapeliwa kizembe wanakuwa kimya na kuugulia maumivu.

"Hao wezi wamekuja na utaratibu huo tumewaelezea wadau ili waelewe utapeli huo tunaendelea kutoa elimu ili wastaafu wetu wasiendelee kutapeliwa na vyombo vya usalama vipo kazini vinashughulikia tatizo hilo ili kukomesha vitendo hivyo," alisema.

Aidha, alisema wastaafu zaidi ya 160,000 wanalipwa kila mwezi pensheni ya Sh. bilioni 67 na rasilimali zilizopo ni Sh trilioni 7.7 na uwezo wa kulipa mafao ya wastaafu wanao bila ucheleweshaji.

Alisema wataafu wanatakiwa kufanya uhakiki wa kila mwaka kuhusu taarifa zao ili wasipate usumbufu kwenye malipo yao ya pensheni.

# LATRA kuzungumza na TIRA wanaopata ajali safirini walipwe

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), imesema inafanya mazungumzo na TIRA ili abiria wanaopata ajali kwenye mabasi safarini wawe wanalipwa.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Habibu Suluo, alisema hayo juzi katika hafla ya kuzindua mitaala ya kufundishia wahudumu katika sekta ya usafiri nchini pamoja na kuwathibitishia madereva.

"Tumeongea na TIRA kwamba watu wanapata ajali nchi hii lakini hawafidiwi. Kwa hiyo tunataka ifike mahali mtu akipata ajali alipwe sababu mabasi yote yana bima," alisema Suluo.

"Na ndiyo maana tunasisitiza matumizi ya tiketi mtandao ambazo zinaingiza abiria kwenye mfumo kwa hiyo ikitokea dharura tunajua abiria walikuwa kina nani. Kwa hiyo hata hii ya kusajili madereva na kuwathibitisha inatupa urahisi wa kuwatambua na kuwasaidia wanapopata tatizo."

"Kanuni ya usafirishaji wa mabasi hairuhusu dereva kusafiri au kuendesha gari kwa zaidi ya saa nane, mfumo tuliouweka kwa sasa unatusaidia kujua kila dereva anayeendesha gari kwa hiyo hata likipata tatizo tunajua."

Alisema takwimu zinaonyesha kuwa ajali nyingi za barabarani zinatokana na sababu za kibinadamu na lengo la kuweka utaratibu wa kuwasajili na kuthibitisha madereva ni kupunguza ajali hizo za barabarani.

"Mwaka 2020 LATRA ilianza kusajili madereva na mwaka 2022 ilitengeneza mfumo wa kielektroniki wa kufanya mitihani ambayo madereva hufanya na wanaofaulu huthibitishwa rasmi na kwa awamu hii ya kwanza madereva 999 wamethibitishwa, utaratibu huu ni endelevu.

Aliwataka madereva kuendelea kujisajili haraka kabla dirisha la kufanya hivyo halijafungwa Julai 31, mwaka huu.

Alisema miongoni mwa faida za kuthibitisha madereva hao ni kuirasimisha fani hiyo, kutambulika kikanda na kimataifa, kuwafungulia fursa kitaifa na kimataifa, kuongeza nidhamu kwa madereva na kuwasaidia kuboresha uchunguzi wa matukio ya ajali.

HABARI MICHEZO

# AZAM YAMKANA LOMALISA, KUMTANGAZA MCAMEROON

**Na Saada Akida**

LICHA ya kuendelea kuhusishwa na mipango ya kuinasa huduma ya beki wa kushoto wa Yanga, Joyce Lomalisa, uongozi wa Klabu ya Azam umefunguka kuwa hauna mpango na nyota huyo wa kimataifa wa DR Congo, huku ukidai unaheshimu mkataba wake.

Kuna tetesi kuwa Azam FC wako kwenye mpango wa kuinasa saini ya beki huyo ili kwenda kuchukua nafasi ya Mzimbabwe Bruce Kangwa, aliyepewa mkono wa kwaheri kuelekea msimu wa 2023/24.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Azam FC, Hashim Ibwe, alisema wanatambua ubora wa beki huyo na wanauheshimu mkataba wake na klabu yake ya sasa.

Alisema hawana mipango ya kumsajili nyota huyo kwa sababu tayari ameshapatikana beki ambaye anakuja kurithi mikoba ya Kangwa na muda wowote watamtambulisha.

"Hakuna ukweli wa Lomalisa kwa sababu mazungumzo yameshaisha na beki kutoka Timu ya Taifa ya Cameroon ambaye alicheza CHAN, safari hii tunasajili wachezaji wanaokuja kuhakikisha tunafikia malengo yetu.

"Wakati wowote tutamtambulisha beki huyo ambaye atakuwa ni usajili wetu wa tatu wa nyota wapya baada ya hapo tutashusha kifaa kingine cha kigeni na tutafunga usajili wetu," alisema Ibwe.

Alisema wanategemea kusajili wachezaji wawili wa kigeni na wamejipanga vizuri kufanya usajili mzuri na wenye malengo kuhakikisha wanakuwa tishio kwa kutwaa mataji msimu ujao.

"Tumejipanga vizuri kwa msimu ujao na ninaimani tutafikia malengo kwa kuwa tumetimiza matakwa ya benchi letu la ufundi linaloongozwa na kocha Youssouph Dabo," alisema ofisa habari huyo.

RASMI...




Kiungo mshambuliaji wa Kimataifa wa Gambia, Gibril Sillah 'The Killer', akikamilisha taratibu za kujiunga na Klabu ya Azam baada ya jana kusaini mkataba wa miaka miwili akitokea Raja Casablanca. Kulia ni Afisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat'. **MPIGAPICHA WETU**

## Dk. Mpango atoa neno kwa JKT, Mashujaa FC

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

MAKAMU wa Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania, Dk. Philip Mpango, ameitaka Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), kuweka mikakati ya kuibua vipaji vya wachezaji chipukizi ili waweze kutoa ushindani kwa klabu kubwa na kongwe nchini, Simba na Yanga pamoja na nyingine zinazoshiriki Ligi Kuu Bara.

Dk. Mpango aliyasema hayo jana wakati wa uzinduzi wa maonyesho ya wiki ya JKT yanayoendelea katika viwanja vya Medeli East vilivyopo jijini Dodoma, yanayoenda sambamba na burudani kutoka kwa bendi za muziki na taarabu kutoka vikundi vya jeshi hilo.

Mpango alisema jeshi hilo lina kila sababu ya kuwekeza kwenye michezo, sanaa na utamaduni kwa sababu wanafursa ya vijana ndani ya jeshi wenye fani mbalimbali za michezo.

Akizungumzia kuhusiana na timu za JKT na Mashujaa zilizopanda Ligi Kuu Bara, Dk. Mpango alisema zinapaswa kusajili wachezaji wazuri ili watoe ushindani mkubwa pindi michuano hiyo itakapoanza.

Alisema Ligi Kuu ya Tanzania kwa sasa iko juu na inaushindani mkubwa, hivyo angependa kuona timu hizo zinatoa ushindani na kubaki nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi hiyo inapofikia ukingoni.

"JKT wekezeni katika michezo, tunahitaji kuona timu ya JKT Ruvu na Mashujaa zinatoa ushindani katika michuano ya Ligi Kuu ya Bara," alisema Mpango.

Aidha, alilitaka mbali na soka kuwekeza pia katika suala la muziki kwa kuwa na bendi zinatoa ushindani dhidi ya zingine za hapa nchini.

Alisema wakifanya hivyo sekta ya michezo hapa nchini itakuwa na ushindani mkubwa na kuzidi kuitangaza nchi katika medani ya michezo kimataifa.

Naye Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Innocent Bashungwa, alisema Jeshi hilo limeweka mikakati katika timu zao za michezo kuhakikisha zinafika mbali kwenye michuano ya kitaifa na kimataifa.

Alisema kwa sasa, timu yao ya JKT Queens inashiriki michuano ya Kimataifa ya Majeshi, hivyo wanaamini na timu nyingine zitatoa ushindani katika mashindano mbalimbali ya michezo zitafanya vizuri.

Kwa upande wa Mkuu wa JKT, Meja Jenerali Rajabu Mabele, alisema jeshi hilo liko imara kwenye sekta ya michezo hususan riadha, soka, mpira wa wavu pamoja na ngumi.

Meja Jenerali Mabele alisema katika kuadhimisha miaka 60 ya JKT tangu ianzishwe wameandaa maonyesho mbalimbali ya michezo zikiwamo burudani kutoka Bendi za Muziki za JKT.

Ukiacha hayo alisema kutakuwa na maonyesho ya wanyama ambayo ni moja ya vivutio vya utalii, hivyo kuwataka Watanzania kujitokeza kwa wingi kwa ajili ya kujionea burudani kutoka JKT.

## Namungo FC yasajili winga, bado straika

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kusajili kiungo kiraka, Erasto Nyoni, Klabu ya Namungo imemsajili mchezaji mwingine anayecheza nafasi ya winga, huku ikisaka straika kutoka ndani na nje ya nchi ili ikamilishe zoezi la usajili msimu huu.

Mwenyekiti wa klabu hiyo, Hassan Zidadu, amesema kwa mujibu wa ripoti ya benchi lao la ufundi hawatokuwa na usajili mkubwa zaidi ya maeneo machache yaliyoainishwa.

Zidadu alisema tayari wameshamsajili mchezaji ambaye anacheza nafasi ya winga, lakini jina lake hawatoliweka hadharani kwa sasa hadi wakamilishe taratibu zote kwa asilimia 100.

"Ripoti ya benchi la ufundi tumeipokea, ipo mikononi mwetu, ilikuwa inaonyesha tuyafanyie kazi maeneo kadhaa lakini ni machache na baadhi tumeshayafanyia kazi, tumemsajili Nyoni na winga mmoja ambaye bado hatujamweka hadharani, muda ukifika tutamtangaza na nafasi iliyobaki kwa sasa ni eneo la straika, mtupiaji mabao ndiyo bado tunamsaka," alisema mwenyekiti huyo.

Zidadu alisema wanachosaka ni uwezo wa kutupia mabao ya si lazima awe mzawa au wa kigeni, hivyo watamsajili yeyote yule ambaye atawaridhisha na atakuwa na uwezo wanaouhitaji.

"Ripoti haikusema ni mzawa au kutoka nje, kwa hiyo ni matakwa na busara yetu sisi wenyewe itatuongoza tukipata wa ndani ambaye atakuwa mzuri zaidi tutafanya hivyo, ila tukikosa hata nje tutatoka," alisema Zidadu.

Alisema wanafanya usajili ambao utawarudisha kwenye chati, au kwenye kiwango ambacho mashabiki wamekizoea na si hiki cha msimu huu.

"Ni kweli hatukuwa kwenye kiwango kizuri msimu huu, lakini hatutaki kuenda huko sana, tumeshajua tatizo ni nini tumerekebisha baadhi ya mambo na tunaendelea kufanyia kazi mengine ikiwamo usajili bora na panapo majaliwa tunataka tena nafasi ya kuiwakilisha nchi kwenye mechi za kimataifa," alisema.

Namungo imemaliza Ligi Kuu msimu huu ikiwa nafasi ya tano, ambayo haikutosha kuifanya kucheza michuano yoyote ya kimataifa, pia ikiondolewa mapema kwenye Kombe la FA.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### KAI ALIPWA ZAIDI ARSENAL

MSHAMBULIAJI wa Ujerumani, Kai Havertz mwenye umri wa miaka 24, amekuwa mchezaji anayelipwa zaidi Arsenal ambapo anachukua pauni milioni 17 kwa mwaka baada ya kujiunga na miaka hiyo akitoka kwa wapinzani wao wa Jiji la London, Chelsea. **(Bild, via Goal)**

### ONANA KUTUA MAN U

MKURUGENZI Mtendaji wa Inter Milan, Beppe Marotta, amethibitisha nia ya Manchester United ya kutaka kumsajili kipa wa klabu hiyo ya Italia na Cameroon, Andre Onana mwenye umri wa miaka 27. **(Mail)**

### BIJLOW NAYE AWINDWA

KLABU ya Manchester United pia inavutiwa na golikipa wa Feyenoord, Mholanzi Justin Bijlow, mwenye umri wa miaka 25, kama mchezaji wao mwingine endapo watamkosa Andre Onana. **(Mirror)**

### TONALI NA NEWCASTLE

MKATABA wa Newcastle United kumsajili kiungo wa kati wa Italia, Sandro Tonali mwenye umri wa miaka 23, kutoka AC Milan unatazamiwa kukamilika, lakini unaweza kucheleweshwa hadi wiki ijayo. **(Fabrizio Romano)**

### UNITED, HOJLUND BADO

DAU la Manchester United la pauni milioni 30 kwa ajili ya mshambuliaji wa Atalanta na Denmark, Rasmus Hojlund, mwenye umri wa miaka 20, limekataliwa. **(Corriere dello sport)**

### GULER ATAJWA MADRID

REAL Madrid inatumaini kushindana na Barcelona katika jitihada za kumsajili kiungo mshambuliaji wa Fenerbahce, Arda Guler. Mchezaji huyo wa Uturuki mwenye umri wa miaka 18, ana kipengele cha kuachiwa kwa pauni milioni 15 katika mkataba wake, ambao utakamilika mwaka 2025. **(Mundo Deportivo)**

### RICE NA WEST HAM

KLABU ya West Ham imemwondoa Declan Rice kama chaguo ambalo mashabiki wanaweza kubinafsisha jezi zao huku mazungumzo ya uhamisho wa pauni milioni 105 na Arsenal kumnunua kiungo huyo wa kati wa England mwenye umri wa miaka 24 yakielekea mwisho. **(Mirror)**

### TIMBER SAFI ARSENAL

MLINZI wa Ajax na Uholanzi, Jurrien Timber mwenye umri wa miaka 22, atakamilisha uhamisho wa kwenda Arsenal wenye thamani ya pauni milioni 45 wiki hii. **(Mirror)**

### COLWILL ASAKWA CHELSEA

MLINZI wa Chelsea mwenye umri wa miaka 20, Levi Colwill anatarajiwa kuwa na jukumu muhimu chini ya kocha mpya Mauricio Pochettino huku, Liverpool na Manchester City zikionesha nia ya kumsaka. **(Football.London)**

### MATA KUONDOKA GALA

KIUNGO wa kati wa zamani wa Hispania, Juan Mata mwenye umri wa miaka 35, ametangaza nia ya kuondoka Galatasaray ya Uturuki. **(Tribal Football)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# INTER YAIONYA CHELSEA MAPEMA KWA LUKAKU

**Hata hivyo, italazimika kutathmini kama atafanya kazi katika mradi wao ili...**

**MILAN, Italia**

MKURUGENZI Mtendaji wa Inter Milan, Beppe Marotta, ameionya Chelsea kwamba haiwezi kudai ada kubwa ili kuachana na mshambuliaji wao, Romelu Lukaku.

Lukaku amerejea Chelsea baada ya mkopo wake na Inter kuisha na pande zote tatu zinataka kufikia makubaliano ambayo yatamfanya Mbelgiji huyo kusalia na 'Nerazzurri' hao kwa mwaka ujao na zaidi.

Chelsea imekataa ofa ya mkopo wa moja kwa moja kutoka kwa Inter na badala yake inashinikiza kuuzwa kwa kudumu msimu huu wa majira ya joto, ingawa maelewano yanaweza kufikiwa juu ya dau la mkopo na jukumu la Inter kumnunua Lukaku msimu wa 2024.

Vyovyote itakavyokuwa, Chelsea wanajiandaa kubeba hasara kubwa kwa Lukaku, ambaye aliigharimu pauni milioni 97.5 alipojiunga nayo mwaka 2021.

"Kwa Lukaku, Chelsea italazimika kutathmini kama anafanya kazi katika mradi wao; kama hafanyi hivyo, mikakati yao inabadilika," alisema Marotta akiiambia Sky Italia. "Ni wazi kuwa hawawezi kufikiria kumweka sokoni na kupokea ofa muhimu.

"Siyo bahati mbaya kwamba uwezekano wa mauzo kwa Saudi Arabia ulikuwa karibu euro milioni 50. Hiyo inaweza kuwa lengo ambalo ni mbali sana na euro milioni 115 tulizoomba, na kupata, kumuuza miaka miwili iliyopita."

Lukaku aliichezea Chelsea mechi 44 katika msimu wake wa kwanza akiwa Stamford Bridge, lakini alichangia mabao 15 pekee na alidai kuwa anataka kurejea Inter miezi michache tu baada ya kuondoka.

Alitumia msimu uliopita kwa mkopo na Inter na Chelsea wako tayari kukata uhusiano wa kudumu msimu huu wa majira ya joto. 'The Blues' walijaribu kumuuza Lukaku Saudi Arabia, lakini alikataa ofa, akisisitiza nia yake ya kurejea Inter.

Msimamo huo umeongeza nia ya Inter kuungana tena na Lukaku, lakini wasiwasi wa kifedha wa Nerazzurri umefanya mazungumzo kuwa magumu hadi sasa.

Hata hivyo, pamoja na kila mtu kufanya kazi kwa lengo moja, maelewano yanatarajiwa kufikiwa hivi karibuni.

# PEPE: HATUKUWA NA UHUSIANO MZURI NA ARTETA

**LONDON, England**

WINGA wa Arsenal, Nicolas Pepe, amekiri uhusiano wake na kocha Mikel Arteta, haukuwa mzuri, lakini alimsifu bosi huyo kwa kujitolea kwake kumsaidia kuwa mchezaji bora.

Pepe alijiunga na Arsenal msimu wa majira ya joto mwaka 2019 kwa ada ya rekodi ya klabu ya euro milioni 72 - rekodi ambayo inatazamiwa kuvunjwa na uhamisho wa Declan Rice wa pauni milioni 105 kwenda hapo Emirates - lakini alishindwa kuonesha kiwango kilichotarajiwa.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ivory Coast, ana mabao 27 na asisti 21 katika mechi 112 alizoichezea Arsenal, lakini mechi 50 kati ya hizo alikuja kama mchezaji wa akiba huku Pepe akihangaika kupata nafasi ya kuanza.

Hapo awali alisajiliwa chini ya kocha Unai Emery, lakini Pepe ametumia muda mwingi wa maisha yake ya uchezaji Arsenal chini ya Arteta, ambaye alijiunga na 'Washikabunduki' hao miezi minne baada ya kuwasili na ripoti zimekuwa zikieleza kwamba wawili hao walikuwa hawaivi kabisa.

Ingawa Pepe amekiri kuwa hakubaliani na maamuzi ya Arteta, lakini alimsifu Mhispania huyo kwa dhamira yake ya kuleta kilicho bora zaidi kutoka kwake.

"Watu wanasema kwamba alinitambua kama mchezaji ambaye hakuwa katika kiwango cha timu yake, katika falsafa yake. Ni uongo kabisa," alisema Pepe kwenye mahojiano na Mail.

"Alipofika, alikuwa na falsafa ya Manchester City. Alikuwa na kikosi kilichojaa ubora katika kila nafasi. Alipozungumza nami, alisema anannitegemea, alitaka nifanye hili au lile.

"Msimu wa kwanza ulipoisha, alizungumza na mimi na kuniambia nifanye hiki au kile, msimu wa pili unakuja, nilikuwa mbadala, nilikuwa nikichanganyikiwa, ningewezaje kuwa mbadala wakati alisema ananihesabia.


"Kila kitu kinazunguka kichwani mwako. Nilikuwa mbadala wa mechi 10. Ilikuwa ni wakati wa kumsajili Willian. Yeye ni namba 10 au winga, lakini anacheza kwenye winga kama namba 11.

"Lakini hilo liliimarika kwa maana ya kwamba alinipa nafasi, nilifunga dhidi ya Sheffield United pale Emirates. Kujiamini kulianza kurejea. Nilianza kuzungumza vizuri.

"Alinisaidia kwa kila hali, kwa kiwango cha mbinu, katika akili ya mchezo kwa sababu falsafa yake inahitaji akili nyingi. Alijua uchezaji wangu si kusubiri kumiliki mpira."

Kwa kuwa Pepe sasa amerejea Arsenal, itabidi uamuzi ufanywe kuhusu mustakabali wake. Winga huyo amebakiza miezi 12 tu kwenye mkataba wake na alikiri kuwa bado hana uhakika wa kuhama kwake.

"Nitarejea Arsenal. Nilitolewa kwa mkopo bila chaguo la kuninunua hivyo lazima nirudi Arsenal."



# Fabregas atundika rasmi daluga

**BARCELONA, Hispania**

KIUNGO wa zamani wa Barcelona na Arsenal, Cesc Fabregas, ametangaza kustaafu kucheza soka akiwa na umri wa miaka 36.

Fabregas amecheza soka kwa muda wa miaka 20 ambao ulimfanya kushinda mataji mengi makubwa alipokuwa Barcelona, Arsenal, Chelsea na Hispania.

"Ni kwa huzuni kubwa kwamba wakati umefika kwangu kutundika viatu vyangu vya kucheza," alisema Fabregas katika taarifa yake kwenye Twitter.

"Kuanzia siku zangu za kwanza Barca, Arsenal, Barca tena, Chelsea, Monaco na Como, nitazithamini zote. Kuanzia kunyanyua Kombe la Dunia, Euro, hadi kushinda kila kitu England na Hispania na karibu mataji yote ya Ulaya, imekuwa safari ambayo sitaisahau kamwe."

Fabregas alitumia muda mwingi wa uchezaji wake akiwa Barca kabla ya kuhamia Arsenal, ambako alicheza mechi yake ya kwanza na kuwa nyota wa klabu alipocheza mechi 303 kati ya mwaka 2003 na 2011.

Kiungo huyo baadaye alirejea Barca ili kujiunga na wachezaji aliowaacha katika ngazi ya vijana, akiwamo Lionel Messi na Gerrard Pique, na kuisaidia klabu hiyo kushinda LaLiga mwaka 2013 pamoja na mataji mawili ya Hispania.

Fabregas alicheza vema katika kiwango cha kimataifa akiwa na Hispania, ambapo alifanikiwa kucheza mechi 110 na alikuwa sehemu muhimu ya kikosi kilichoshinda mataji mawili ya Euro na Kombe la Dunia la mwaka 2010.

Mwaka 2015, Fabregas alihamia Chelsea ambapo alikaa miaka mitano, akishinda mara mbili Ligi Kuu pamoja na Kombe la FA na Ligi ya Europa.

Aliondoka Stamford Bridge mwaka 2019 na tangu wakati huo alifurahia vipindi akiwa na AS Monaco na timu ya Serie B ya Como.

## Thuram atua Inter kwa uhamisho huru

**MILAN, Italia**

KLABU ya Inter Milan imekamilisha usajili wa mshambuliaji wa Mfaransa, Marcus Thuram, kwa uhamisho wa bure kutoka Borussia Monchengladbach, klabu hiyo ya Serie A imetangaza.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, ni mtoto wa mshindi wa Kombe la Dunia na Ufaransa, Lilian Thuram, na anajiunga na Inter baada ya misimu minne na Gladbach ambapo alifunga mabao 44 na kusajili asisti 29 katika mechi 134.

Thuram ameichezea Ufaransa mara 10, baada ya kucheza kwa mara ya kwanza katika timu ya wakubwa mwaka 2020 na alikuwa sehemu ya kikosi chao cha euro mwaka huo.

Alicheza pia Kombe la Dunia mwaka jana, ambapo Ufaransa ilimaliza kama washindi wa pili.

"Marcus Thuram ni mwepesi. Daima amekuwa mwepesi kufikia malengo yake na kushinda kikwazo chochote katika njia yake. Kuonesha kwamba ana thamani kubwa zaidi ya jina lililo nyuma ya jezi yake," ilisema taarifa ya Inter.

Thuram, ambaye alizaliwa jijini Parma wakati baba yake alipokuwa katika klabu hiyo ya Italia, alihusishwa na klabu kadhaa za Ulaya kabla ya kusajiliwa na Inter.

Inter, ambao walifungwa na Manchester City katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwezi uliopita, tayari wametangaza kuondoka kwa Milan Skriniar, Danilo D'Ambrosio na Roberto Gagliardini baada ya mikataba yao kumalizika.



# KOCHA WA AZAM FC ANUKIA COASTAL UNION

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kulivunja benchi la ufundi hivi karibuni, Klabu ya Coastal Union, imetajwa kuwa iko mbioni kumshusha kocha wa zamani wa Azam FC, Abdihamid Moallin.

Hata hivyo, mwenyewe hakukubali wala kukanusha, huku kukiwa na taarifa kwamba ana mazungumzo na klabu zingine za hapa nchini.

"Sijasaini mkataba na klabu yoyote Tanzania, ila ni kweli niko kwenye mazungumzo na baadhi ya klabu hivyo tusubiri kwanza," alisema.

Habari zinaeleza kuwa Coastal Union ni moja kati ya klabu zilizofanya mazungumzo na kocha huyo, lakini zipo zingine zinazomhitaji, hivyo mwenye kisu kikali ndiye atakayekula nyama.

Moallin alitua nchini akiwa Mkurugenzi wa Ufundi wa Azam FC kabla ya kupewa kibarua cha kuinoa timu ya wakubwa Januari mwaka jana akichukua nafasi ya Mzambia George Lwandamina, ambaye alitimuliwa, lakini na yeye alifungashiwa virago Agosti mwaka jana, na nafasi yake kuchukuliwa na Mfaransa Denis Lavagne ambaye naye hakudumu.

Kwa upande wa Coastal Union, Katibu Mkuu Omary Ayoub, aliwataka mashabiki wa klabu hiyo kutokuwa na wasiwasi na kufadhaika kwa kile walichokifanya kuvunja benchi lote la ufundi, kwani wanataka kutengeneza lingine imara, ikiwamo kufanya usajili wa wachezaji bora kuepuka kucheza kwa presha zaidi badala ya kutumia ufundi.

"Nawaambia mashabiki wa Coastal Union, mambo mazuri yanakuja, hiki ambacho tumekifanya, tutaleta watu ambao tunaamini watakuwa na msaada mkubwa kwenye benchi pamoja na usajili wa wachezaji wengine wenye uwezo na uchungu na klabu yetu," alisema.



Abdihamid Moallin

# Tabora Utd kutambulisha majembe yao Jumatano

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Tabora United (zamani Kitayosce), keshokutwa, Jumatano inatarajia kutambulisha wachezaji wake wapya itakaowatumia kwa ajili ya msimu ujao wa mashindano, imeelezwa.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Pendo Lema, amesema jana kuwa tayari wameshamaliza kufanya usajili na sasa wanachofanya ni kujiandaa kuwatambulisha tu.

"Tutakuja kutangaza Julai 5 wachezaji wetu tuliowasajili kwa ajili ya msimu ujao, sisi tulianza kufanya maandalizi ya usajili mapema tu tulipopanda daraja," alisema ofisa huyo.

Pendo alisema wamefanya usajili kwa ajili ya kuleta chachu kwenye Ligi Kuu na wala si kwa kusindikiza, hivyo kuzitaka timu zote kujiandaa kwa upinzani mkali.

"Hatukusajili tu mradi tumesajili, tumesajili wachezaji haswa, kwanza tunao wachezaji wazuri ambao wametupandisha daraja, lakini tumesajili wengine wapya kimyakimya na wakati huu ambao wengine wanapigana vikumbo sisi tayari siku nyingi tumeshamaliza," alisema.

Timu hiyo ilipanda Ligi Kuu wakati ikiitwa Kitayosce, na ilimaliza nafasi ya pili ikiwa na pointi 60 chini ya JKT Tanzania.

Mbali na Kitayosce na JKT Tanzania, timu nyingine kutoka Ligi ya Championship iliyopanda Ligi Kuu ni Mashujaa FC ambayo yenyewe ilibidi isubiri mpaka mechi ya 'play off', ikiibwaga Mbeya City kwa jumla ya mabao 4-1, ikishinda 3-1 nyumbani na bao 1-0 ugenini.

# Yanga sc kuiboma tena ASEC Mimosas

INATOKA UK. 24

kupambana ili wabaki tena kwa ajili ya msimu ujao.

Tayari imeshapata Kocha Mkuu raia wa Argentina, Miguel Angel Gamondi, ambaye ameahidi kuja nchini mapema kwa ajili ya kuanza kukiandaa kikosi chake.

# Simba yageukia viungo wakabaji

INATOKA UK. 24

"Hatutaki kurudia makosa ya msimu uliopita unamkosa huyu, unaanza tena mazungumzo na mtu mwingine, yanakuwa marefu mpaka kikosi kinaanza maandalizi ya msimu ujao bado hatujamaliza kusajili, tunataka mwalimu akianza awe na wachezaji wote anaowahitaji," chanzo kilibainisha.

Simba inataka kutibu tatizo sugu la kiungo mkabaji ambapo kwa sasa inawategemea wachezaji wawili tu, Sadio Kanoute raia wa Mali na Mtanzania Mzamiru Yassin ambao hata hivyo, wataalamu wa soka wanasema si viungo wakabaji asilia, badala yake ni wasaidizi wa viungo wakabaji wanaocheza juu kidogo.

Tangu kuondoka kwa Mbrazil James Kotei, Gerson Fraga na Thadeo Lwanga, ambao ndiyo viungo wakabaji asilia, Simba imekuwa na tatizo hilo ambalo limekuwa likiigharimu katika baadhi ya mechi.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema safari hii hawataki tena kufanya makosa yaliyowagharimu ndiyo maana wanasajili wachezaji ambao wana mikataba na klabu zao.

Amesema pesa kwao si tatizo na kwamba watamnunua mchezaji yeyote kwa gharama yoyote kutoka mahala popote.

"Mzigo upo, tutamsajili yeyote yule, mradi tu kocha Robertinho (Robert Oliveira) amempendekeza," alisema.

Kwa mujibu wa Ahmed, kuanzia leo Jumatatu klabu hiyo inaweza kuanza kutangaza wachezaji ambao imeshawasajili mpaka sasa.

# Michezo

Jumatatu Julai 3, 2023

Nipashe




Inter yaionya Chelsea mapema kwa Lukaku UKURASA 21

# YANGA SC KUIBOMOA TENA ASEC MIMOSAS

## Ni wakati Mayele, Lomalisa wakiendelea kuipasua kichwa kuondoka, yarudi Ivory Coast kumshusha...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Klabu ya Yanga leo ikiwa na mkutano na waandishi wa habari, inaelezwa ipo mbioni kuibomoa kwa mara ya pili ASEC Mimosas ya Ivory Coast kwa kumchukua kiungo wao, Zoungrana Mohamed, raia wa Ivory Coast, kama ilivyofanya msimu uliopita kwa Stephane Aziz Ki.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, jana aliliambia Nipashe kuwa leo wanakwenda kuongeza mambo makubwa zaidi kuliko ya juzi, huku taarifa zikidai wako kwenye harakati za kumtwaa kiungo huyo wa kukaba kwenda kuungana na kina Yannick Bangala, Mudathir Yahaya na wengine.

Taarifa zanadai mchezaji huyo wa kigeni anakuja kuchukua nafasi ya Mamadou Doumbia, ambaye wapo katika mchakato wa kuachana na wakati wowote atapewa mkono wa kwaheri baada ya kutowaridhisha si tu watu wa benchi la ufundi, bali hata wanachama na mashabiki wa Yanga.

"Anasajiliwa kiungo huyo kuchukua nafasi ya Doumbia na inavyoonekana hakuna mpango wa kusajili beki wa kati, tuna imani na Dickson Job, Bakari Mwamnyeto, Ibrahim Abdallah 'Bacca' na hata Bangala huwa anacheza beki wa kati, kwa hiyo akili sasa ipo kwenye maeneo mengine," kilisema chanzo.

Kabla ya kumleta mchezaji huyo, Yanga italazimika kumlipa mchezaji huyo raia wa Mali kiasi cha dola 50,000, zaidi ya Sh. milioni 150,000 za Kitanzania.

Msimu uliopita Yanga ilifanikiwa kumsajili Aziz Ki kutoka klabu hiyo ya Ivory Coast ikiwa moja ya sajili zilizoshangaza na kushtua nchi.

**Hata hivyo, habari zinasema kuwa msimu huu Yanga haitosajili wachezaji wengi kutokana na kuwa na uhakika wa kuwabakisha ambao waliiletea mafanikio makubwa, kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kombe la FA na kufika fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika.**

Baada ya kuondoka kwa Kocha Mkuu, Nasreddine Nabi, ilionekana klabu hiyo ingepoteza wachezaji wengi, kama vile Djuma Shaaban, Bangala, Fiston Mayele, Joyce Lomalisa, lakini imefanikiwa kuwatuliza baadhi na wengine ikipambana kuwabakisha.

Imeelezwa wachezaji Lomalisa na Mayele ndio kwa kiasi kikubwa bado wanaendelea

INAENDELEA UK. 23



Zoungrana

# Simba yageukia viungo wakabaji

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Simba ipo kwenye mazungumzo na viungo wakabaji watatu kutoka nje ya nchi kwa ajili ya kutibu tatizo hilo sugu la muda mrefu.

Simba ambayo licha ya kwamba hajathibitisha rasmi, lakini taarifa zimedai imeshawasainisha wachezaji wawili raia wa Cameroon, winga wa kushoto, Lendre Onana aliyekuwa akiichezea Rayon Sport ya Rwanda na beki wa kati, Che Fondoh Malone kutoka Coton Sport, huku pia ikidaiwa kuwa kwenye hatua za mwisho kumsajili kipa Mbrazil, Caique Luiz Santos anayekipiga na Ypiranga SC, lakini kwa sasa ikigeukia eneo la kiungo mkabaji.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zimesema kuwa iko kwenye mazungumzo na wachezaji watatu wanaocheza eneo hilo, ambao ni Efoe Novon kutoka ASKO Cara ya Togo, Harvy Ossete raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo anayeichezea FC Saint Eloi Lupopo, na Banfa Sylla wa MAS Fes ya Morocco.

Hata hivyo, inadaiwa mabosi wa Simba na kocha wao, Robert Oliveira, wanavutiwa zaidi na Sylla, ambaye thamani yake inatajwa kuwa ni dola za Kimarekani 170,000 ili kuvunja mkataba kwa klabu yake.

"Lengo ni kumpata Sylla, lakini hawa wengine nao si wabaya, ni wachezaji wazuri sana na tumewajumuisha ikiwa ni kama mbadala iwapo dili halitofanikiwa, kwenye soka kuna mambo mengi, mnaweza kuongea vizuri, lakini mwishoni mambo yasiende vizuri, uzuri ni kwamba wote wameshazungumza nao," kilisema chanzo kutoka ndani ya klabu hiyo.

Chanzo hicho kimesema kutokana na muda kuwa mfupi, imebidi wafanye haraka kumaliza usajili ili kikosi kiingine kambini mara moja kwa ajili ya kujiandaa na msimu mpya (preseason), hivyo wamewaweka tayari wachezaji wote hao watatu ili sehemu moja ikishindikana, basi mwingine anachukua nafasi.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >